**RAIS** Samia ajadiliana na viongozi wa sekta binafsi Ikulu

UKURASA 3



**MZEE** Mwinyi aeleza umuhimu wa kuwapo kwa vyama vya upinzani

UKURASA 4


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Mambo kuvuta w/ulemavu kupenda shule ni haya hapa
'Hakuna hedhi salama kwani mabinti wanafunzwa na dunia'
ELIMU
NA SABATO KASIKA
WILAYA YAPANIA KUTISHA KISAYANSI
▪Yaja na shule maalum ya wavulana wanasayansi

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Juni 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580598

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710


# Mitihani inayomkabili DCI mpya Wambura hii

UKURASA 2




Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camilius Wambura,

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WAATHIRIKA MOSHI WA TUMBAKU KUTOKA KWA WAVUTAJI WAONGEZEKA

TAKRIBANI watu milioni sita, hufariki dunia kila mwaka duniani kutokana na matumizi...

UKURASA WA 7

### ANAYEDAIWA JAMBAZI SUGU AUAWA

MTU anayedaiwa kuwa jambazi sugu, Iddi Masasi (43), ameuawa kwa kupigwa risasi wakati akijaribu kuwakimbia polisi waliokuwa wakimsaka...

## SWEDEN KUTOA MABILIONI KWA FAMILIA MASKINI

UKURASA 4

# Bulaya: Serikali isigeuke mwiba kwa vyombo habari

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAMADOU SAKHO ALETA NEEMA SOKA ZANZIBAR** UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK. 6



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Equity Bank, Esther Kitoka (kushoto), akimkabidhi cheti cha ushiriki kwa mwanachama wa kikundi cha Faith Vicoba Group katika sherehe za miaka mitano ya kikundi hicho iliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mitihani inayomkabili DCI mpya Wambura

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI mpya wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camilius Wambura, anashika usukani huku akikabiliwa na mitihani wa kuibuka kwa matukio ya uhalifu katika miji na majiji na lawama zikielekezwa kwa baadhi ya askari kutoa siri za matukio yanayopelelezwa.

Kibarua kikubwa kinacho mkabili ni cha kukidhi dhima ya kisheria ya uanzishwaji wa jeshi hilo la ulinzi wa raia na mali zao, huku na matakwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alipokuwa akizungumza na wazee wa jijini Dar es Salaam, alilinyooshea kidole Jeshi la Polisi dhidi ya kuongezeka kwa matukio ya uhalifu nchini.

Wambura ambaye kabla ya kushika nafasi hiyo Mei 18, mwaka huu, alipandishwa cheo na kuwa Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, nafasi aliyoitumikiwa kwa siku 14 kabla ya kuteuliwa tena kushika nafasi hiyo ya juu.

Mitihani iliyo mbele yake ni pamoja na kukabiliana na wizi wa kutumia silaha, makosa mtandaoni (ikiwamo ujumbe unaotumwa na matapeli wa 'tuma pesa kwa namba hii'), wizi majumbani, wizi wa magari na vifaa vya magari, uporaji, utekaji na shughuli za kisiasa.

Juzi taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Ikulu, ilisema Rais Samia amemteua Wambura kuwa Kamishna wa Polisi (CP) na kumpandisha cheo kuwa DCI.

Mtihani kwa DCI unaonekana kwa kuwa ndani ya muda mfupi anatakiwa kuonyesha namna ofisi yake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wamejipanga kupambana na uhalifu nchini ili kutimiza dhima ya uanzishwaji wake.

**MATUKIO YALIYOTIKISA**

Matukio mengi yametikisa Dar es Saalam kwa mwezi Aprili na Mei, mwaka huu, huku uhalifu wa kuiba vifaa vya magari, magari na wizi majumbani ukishika kasi, kiasi cha baadhi ya watu kupoteza maisha.

Machi 18, mwaka huu, watu watano wanaosadikiwa ni majambazi walimvamia Mkurugenzi wa Benki ya Azania nyumbani kwake Mbweni Mpiji, Dar es Salaam, na kuwashambulia walinzi na kisha kuwapora silaha aina ya Shotgun Pump Action ikiwa na risasi tano.

Mei 8, mwaka huu, Polisi walidai kuwa baada ya uporaji wa silaha hiyo waliitumia kuvamia baa moja iliyopo Mikocheni A na kumshambulia na kumuua mlinzi, Regan Sylivester.

Mei 7, mwaka huu, watuhumiwa hao wanadaiwa kuvamia kituo cha kuuza mafuta kilichopo Mabwepande na kuwashambulia walinzi, wahudumu na wateja, kisha kupora Sh. milioni 2.4 pamoja na silaha aina ya Shotgun iliyokuwa ikitumiwa na walinzi.

Mei 25, mwaka huu, maeneo ya Mabibo watu wanaosadikiwa majambazi walimpiga risasi na kumjeruhi mfanyabiashara.

Mei 23, mwaka huu, watu wanaosadikiwa kuwa ni majambazi watano walivunja nyumba ya Daud Ramadhan, Mikocheni A na kuiba vitu vya ndani televisheni moja, simu mbili, kompyuta mpakato mbili, poko (mouse) za kompyuta nne.

Mei 23, mwaka huu, mtu mmoja Kilambo Obale na wenzake walivamia nyumba ya mstaafu wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Milton Lazaro, mkazi wa Masaki na kuiba televisheni, kompyuta na fedha za Canada Dola 2,700 pamoja na silaha aina ya shotgun.

Mei 15, mwaka huu, huko Kibaha watu wanaosadikiwa kuwa ni majambazi waliiba pikipiki yenye namba za usajili MC 136 CSA na kupelekwa mkoani Morogoro.

Tukio jingine ni watu wanne wanaosadikiwa kuwa ni majambazi waliiba magari manne maeneo ya Kinondoni na Ilala, Dar es Salaam.

Katika matukio hayo Polisi ilieleza kukamata watuhumiwa 25 kwa nyakati tofauti wakiwa na vithibitisho na hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi yao na lilieleza kuwa linaendelea kufanya upelelezi ili kuwabaini wahusika wa matukio ya kihalifu nchini.

April 25, mwaka huu, Jeshi hilo Dar es Salaam, lilieleza kukamata watuhumiwa 49 pamoja na gari walilokuwa wakilitumia kufanya matukio ya wizi na ununuzi wa vifaa vya wizi.

**MIKOA YENYE HISTORIA YA UHALIFU**

Aidha, DCI ana kibarua cha kudhibiti kurejea kwa matukio ya uhalifu mkubwa wa kutumia silaha uliohusisha raia Kenya, Uganda na Tanzania, hasa kupora kwenye benki na maduka ya kubadilishia fedha mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Dar es Salaam na kiasi kikubwa kuwahi kuibwa katika benki ya NBC, Sh. bilioni 3.3.

Uhalifu huo ulitikisa Kanda ya Kaskazini mwaka 2004 hadi 2015, kiasi cha baadhi ya watu wanaodaiwa kufadhili mtandao wa uhalifu nchini, kukamatwa na kutakiwa kukiri kutoendelea na kazi hiyo na kazi hiyo ilifanywa na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Venance Tosi, baadaye Kamanda Robert Boaz, aliyekuwa RPC mkoa huo alipandishwa kuwa DCI.

Mikoa mingine ni Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mtwara, Kigoma na Pwani.

**RAIS SAMIA**

Mei 7, mwaka huu, Rais Samia akizungumza na wazee wa Dar es Salaam, alionyesha kukerwa na kuibuka upya kwa matukio ya uahlifu na kulionya Jeshi la Polisi na wanaofanya matukio hayo.

"Dar es Salaam sasa wanajaribu kina cha maji kuna viujambazi, viupokonyaji vimeanza kuja juu, hivyo naomba niteo ujumbe kuwa wasijaribu kina cha maji Mkuu wa Polisi Nchini (IGP) naomba ukalisimamie hilo," alisema.

UTEUZI

Pamoja na Wambura wengine waliopandishwa cheo ni ni Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Hamad Khamis Hamad, kuwa Kamishna wa Polisi (CP) pia amemteua kuwa Mkuu wa Kamisheni ya Fedha na Lojistiki Polisi nchini na kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa makosa ya jinai Makao Makuu ya Polisi Zanzibar.

**ATENGUA**

Rais Samia alitengua uteuzi wa aliyekuwa Katibu Tawala wa Simiyu Azza na kumteua Prisca Kayombo, kuwa Katibu Tawala wa mkoa huo na kabla ya uteuzi huo alikuwa ofisa mkuu wa utawala na utumishi katika Wizara ya Fedha na Mipango, wataapishwa leo.

## Bili ya maji yamweka matatani ofisa biashara

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

OFISA Biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, Anthony Marco, amejikuta matatani, baada ya kutuhumiwa kutumia maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 23.6 kwenye shamba lake la vitunguu lenye ukubwa wa hekari 13 bila kulipia ankara ya matumizi hayo tangu mwaka 2020.

Kukamatwa kwa ofisa huyo kunatokana na operesheni iliyofanywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga (IGUWASA) kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo.

Mkurugenzi wa IGUWASA Wilaya ya Igunga, Hussein Salumu Nyembea, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo, na kwamba mtumishi huyo wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga alikuwa akitumia mita mbili katika shamba lake la vitunguu lililopo Mtaa wa Masanga lenye ukubwa wa hekari 13.

Aidha Nyembea alibainisha kwamba mtuhumiwa aliomba kufungiwa mita mbili kwenye eneo hilo la shamba lake kama wateja wengine na kwamba tangu alipofungiwa mita hizo mwaka jana, hajawahi kulipa ankara ya matumizi ya maji, huku akiendelea kutumia kumwagilia hekari zake 13 za vitunguu.

Alifafanua kwamba baada ya kubaini hali hiyo, katika msako unaoendelea wa nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa ndipo alipofanyiwa hesabu ya matumizi ya maji aliyotumia kwa muda wote huo, ambayo yalifikia zaidi ya shilingi milioni 23.6.

Alisema aliposikia msako alikimbilia katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuomba msaada, ambao hata hivyo Mkuu wa Wilaya ya Igunga, John Mwaipopo alimrudisha kwenye ofisi za Iguwasa ili wakaelewane.

Alisema wakati wakiwa akatika ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ndipo mtumishi huyo alionekana kuomba msaada, lakini Mkurugenzi wa Iguwasa alitaka kulipwa kiasi chote cha fedha alizokuwa akidaiwa mtuhumiwa.

Hata hivyo mkurugenzi huyo alisema baada ya kubanwa ndipo mtumishi huyo alilipa shilingi milioni tatu na kubakiza deni la zaidi ya shilingi milioni 20.6 na kuahidi kwa maandishi kuwa atakuwa akilipa deni hilo shilingi 500,000 kila wiki hadi atakapokamilisha kulipa deni lote hilo.

## HABARI KITAIFA

# Ester Bulaya: Serikali isigeuke mwiba kwa vyombo vya habari

**Na Romana Mallya**



MBUNGE wa Viti Maalum, Ester Bulaya, amesema vyombo vya habari vinafanya kazi sawa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali (CAG) na kuitaka serikali kupanua zaidi wigo wa kutekeleza majukumu yao.

Bulaya aliyasema hayo jana bungeni wakati akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2021/2022.

"Tabia ya kufungia vyombo vya habari tukubali tukatae vyombo vya habari ni CAG mwingine tusitake kutolewa habari za kufurahisha lazima tukubali na kukosolewa zote ni habari za kujenga taifa letu.

"Ni kweli soko la magazeti limekufa kwa sababu wengi hawayanunui kwa sababu wanaona habari ni zile zile na habari za uchunguzi zimepungua, makala za uchunguzi zimepungua, hata ukienda kwenye mijadala angalia tathmini zinazotolewa watu wanazitoa kwa hofu."

Bulaya alisema hawasemi hakuna uhuru usio kuwa na mipaka, lakini wakiwahakikishia waandishi wa habari wafanye kazi zao kwa weledi na magazeti yasifungiwe ovyo.

"Mheshimiwa Waziri ukifungia maana yake umesimamisha zaidi ya familia 50, zaidi ya wafanyakazi 50 hawana ajira, ina maana watoto hawaendi shule unaweka familia katika hali ngumu, faini imekuwa chanzo cha mapato, watu wanazungumzia kwenye michezo hata huku kwenye magazeti na vyombo vya habari kiujumla kuna shida, mtoze faini kidogo ajirekebishe lakini kisiwe chanzo cha mapato," alisema.

Mbunge huyo alisema licha ya kufanya kazi kubwa ya kuelimisha umma, hali ya wanahabari kiuchumi ni duni na wanafanya kazi kwenye mazingira ya kubanwa.

"Mimi ni mwanahabari nimefanya kazi chumba cha habari takribani miaka sita, nimeona watu wengi wamejikita katika michango ya michezo, lakini mheshimiwa Waziri (Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa) waandishi wako wa habari wanalipwa vibaya sana.

"Waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana na taifa letu linawategemea kuielimisha jamii, lakini wamekuwa waslahi yao ni madogo sana ni wa vyombo vya serikali na vyombo vya habari binafsi siyo walioajiriwa tu mishahara yao midogo haiongezwi hata waandishi wa kujitegemea nao wanalipwa vibaya na hawana watu wa kuwasemea," alisema.

Pia alisema kila kinachokatwa kwenye mishahara yao hakipelekwi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mbunge wa Mafinga, Cosato Chumi, alisema kuna haja ya serikali kusaidia sekta ya habari na rasilimali ili wafanye kazi kwa uhuru.

"Wanahabari wanafanya kazi nzuri kuna haja ya kuwawezesha tuchukulie mfano gazeti la serikali, nimeambiwa linadai taasisi mbalimbali za serikali mabilioni ya fedha kwa mtindo huu haliwezi kushindana," alisema.

# Rais Samia akutana na viongozi wa sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

**Viongozi hao walimwahidi Rais Samia kuwa wapo tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha wanakuza zaidi uzalishaji kupitia sekta mbalimbali ili kukuza uchumi wa nchi, kuzalisha ajira na kuinua ustawi wa jamii.**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na viongozi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), na kuzungumza nao kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu kukuza biashara na uwekezaji pamoja na kupanua wigo wa kodi.

Mkutano huo ulifanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana, ambapo viongozi hao walimshukuru Rais Samia kwa hatua alizoanza kuchukua hatua kuimarisha uhusiano kati ya serikali na sekta binafsi.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema sekta binafsi imeanza kuona matokeo ya juhudi za Rais Samia, ambapo kufuatia ziara ya Kenya, sekta binafsi ya Kenya na sekta binafsi ya Tanzania wamekubaliana kuanzisha soko la pamoja la bidhaa ambalo litawawezesha wafanyabiashara wa pande zote kuuza na kununua bidhaa sokoni hapo na pia mpango wa bajeti ya mwaka 2021/22 umezingatia maoni ya sekta binafsi.

Hata hivyo, viongozi hao wameomba serikali kuendelea kutilia mkazo juhudi za kuboresha zaidi mazingira ya kufanya biashara (Blue Print), kusimamia ulipaji wa kodi, kusimamia manufaa ya ndani (local content) katika miradi mikubwa, kufanya utafiti, kuvutia mitaji, uwekezaji katika maeneo ya kimkakati na kutilia mkazo kuendeleza kilimo ambacho kinaajiri Watanzania wengi.

Viongozi hao walimwahidi Rais Samia kuwa wapo tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha wanakuza zaidi uzalishaji kupitia sekta mbalimbali ili kukuza uchumi wa nchi, kuzalisha ajira na kuinua ustawi wa jamii.

Kwa upande wake, Rais Samia aliwapongeza viongozi hao kwa juhudi kubwa zinazofanywa na TPSF kuitikia wito wake wa kutekeleza jukumu la kukuza uchumi na amewahakikishia kuwa serikali itawaunga mkono katika juhudi hizo.

Rais Samia aliahidi kufanyia kazi maoni yao pamoja na maoni mengine yatakayotolewa katika mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) unaotarajiwa kufanyika Juni, 2021.



# Sweden kusaidia kaya maskini kwa bil. 130/-

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya Sweden imesema inatarajia kutoa Sh. bilioni 130 kwa ajili ya kusaidia mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Ahadi hiyo ilitolewa na Katibu wa Miradi ya Maendeleo ya Ushirikiano wa Kimataifa wa serikali ya Sweden, Junine Aricson, alipotembelea walengwa wa mpango huo wa kunusuru kaya maskini Kivule Majohe, Ilala jijini Dar es Salaam. Alisema katika kipindi cha kwanza cha TASAF awamu ya tatu kilichomalizika mwaka jana, serikali hiyo ilitoa Sh. bilioni 200.

"Katika kipindi cha kwanza cha mpango huu wa tatu wa TASAF, Sweden tulichangia Sh. bilioni 200 lakini katika awamu hii tumepanga kuchangia Sh. bilioni 120 na tutazitoa ndani ya siku chache zijazo," alisema Ericson.

Alisema wanapata moyo wa kuchangia mpango huo kwa sababu wameshuhudia namna unavyosaidia kubadilisha maisha wa wananchi wenye hali ya chini.

"Sisi kama Sweden, tunapata moyo na nguvu ya kuendelea kuchangia kwenye mpango huu kwa sababu tumeona matunda yake, tumekuwa tukitembelea walengwa, kuwasikiliza namna ambavyo walikuwa wakiishi maisha duni kabla ya mpango, lakini kwa sasa maisha yao yamebadilika kwa kiwango kikubwa," alisema.

'Tunataka kuona idadi kubwa ya wananchi walio katika maisha ya chini wanaondokana na umaskini, tunataka kuona watoto wao wanapata huduma zote za msingi na wanaishi katika maisha bora."

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema mpango huo umesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha maisha ya walengwa hao, na kwamba walengwa 1992 wamejitoa kwa hiari baada ya kujimudu kimaisha kutokana na mpango huo.

"Kwa kweli mpaka kufikia hapa tulipo ni jambo la kumshukuru Mungu, mpango huu umeonyesha impact kubwa hasa kwa walengwa, wapo ambao wamegraduate na kutoka kwa hiari kwenye mpango baada ya kuona kwamba sasa wanaweza kusimama wenyewe, wawapishe na wenzao ni mafanikio makubwa sana," alisema Mwamanga.

"Kila mara tumekuwa tukiwaelimisha kwamba, wanaposaidiwa na mpango, wajifunze pia namna ya kuendesha miradi midogo na waweke akiba na ndivyo wamekuwa wakifanya na tunashukuru kwamba wamefika katika hatua ya kuona hapo walipofikia wao ni angalau, sasa wawapishe na wengine au wagraduate, hilo ni jambo jema."

Mmoja wa walengwa kutoka katika kikundi cha Kondeni ambacho kimeundwa na wanawake walio katika mpango huo kwa ajili ya kujiwekea akiba na kufanya shughuli za ujasiriamali, Tausi Salumu, alisema TASAF imewakomboa hali ya kujiona hawawezi na sasa wamepiga hatua kubwa kupitia elimu ya ujasiriamali wanayopewa na kuanzisha vikundi.



Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo TIB, Sonia Mlaki, akipokea zawadi ya mshindi wa kwanza kwa upande wa taasisi za kifedha kutoka kwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exahud Silaoneka Kigahe. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima (wapili kulia). Kushoto ni Kaimu Katibu Tawala mkoani Tanga, Kasunzu Rashid na Mwenyekiti wa TCCIA Chemba ya Tanga, Rashid Mwanyoka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi aeleza umuhimu wa upinzani

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema mfumo wa vyama vingi ulioanzishwa wakati akiwa madarakani, ulilenga kukuza demokrasia.

Amesema jukumu la chama tawala wakati huo, ilikuwa ni kuwa na jukumu la kuwatumia wapinzani kama kioo cha kuonea kasoro zilizohitaji kushughulikiwa.

Mzee Mwinyi, anasimulia hayo kwenye kitabu chake, kiitwacho 'Mzee Rukhsa. Safari ya Maisha Yangu'.

Mzee Mwinyi anasema wakati wa mwaka 1991, kulikuwapo mjadala wa kitaifa kuhusu mustakabali wa taifa kisiasa, hususan mfumo wa siasa nchini kwa siku zijazo.

"Wananchi kwenye pembe zote walishiriki mjadala na kutoa maoni yao iwapo Tanzania ibakie na nchi ya chama kimoja cha siasa au turuhusu mfumo wa vyama vingi. Tuliunda tume ya rais kuratibu mjadala na maoni;

Ripoti ya awali ya tume ilikabidhiwa kwangu na mwishoni mwa mwaka huo (1991), nami nikaagiza vikao vya CCM kujadili yaliyokuwamo."

Mzee Mwinyi anasema alipoipokea ripoti ya mwisho, aliagiza kuwasilishwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Aprili mwaka 1992, na kwamba huo ukawa ni mwanzo wa nchi kurejea mfumo wa vyama vingi baada ya kupita miaka 30 ya chama kimoja.

"Nikitazama nyuma, naridhika kuwa Tanzania ilijiandaa vizuri sana kusimamia vizuri kwa umakini mkubwa mageuzi kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda kwenye mfumo wa vyama vingi.

"Nchi inapofanya mabadiliko makubwa namna hii ni vyema kuwa makini na kwenda polepole, ukianza kujenga msingi imara, kisha kupandisha kuta, hatimaye kuweka paa," anasema Mzee Mwinyi.

Anasema hadi hivi sasa ina mfumo huo unaoimarika, nchi ikitulia bila kuathiri tunu za amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

# Waathirika moshi wa tumbaku kutoka kwa wavutaji waongezeka

**Na Christina Mwakangale**

TAKRIBANI watu milioni sita, hufariki dunia kila mwaka duniani kutokana na matumizi ya tumbaku au kukaa karibu na mvutaji.

Pia idadi hiyo huchangia asilimia sita ya vifo vya wanawake, asilimia 12 ya wanaume na 28 ni watoto.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na inakadiriwa ifikapo mwaka 2030 vifo vitokanavyo na matumizi ya tumbaku vitafikia zaidi ya milioni nane.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo katika taarifa yake, jana, kuhusu Siku ya Kutokuvuta Tumbaku Duniani, inayoadhimishwa Mei 31, kila mwaka. Alisema nchini wastani wa asilimia 14 ya Watanzania wanatumia tumbaku.

Dk. Gwajima alisema idadi ya wanaoathirika kutokana na moshi wa tumbaku toka kwa wavutaji, inaongezeka na asilimia 17.5 huathiriwa na wanaovuta sigara majumbani na asilimia 24.9 sehemu za kazi.

Alisema takwimu hizo ni baada ya utafiti kufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kushirikiana na WHO, kutathmini viashiria hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema utafiti huo ulionyesha, kati ya Watanzania hao, wanaume ni 26.0 na wanawake ni asilimia 2.9 na kwamba athari ya uvutaji tumbaku, hupunguza kiwango cha oksijeni inayosafirishwa na damu na kusababisha damu kuganda.

"Takribani watu milioni sita, hufariki kutokana na matumizi ya tumbaku au kukaa karibu na mvutaji, huchangia asilimia sita ya vifo vya wanawake na asilimia 12 vya wanaume kwa mwaka. Inakadiriwa ifikapo mwaka 2030, vifo vitokanavyo na matumizi ya tumbaku vitaongezeka na kufikia zaidi ya milioni nane kwa mwaka," alisema Dk. Gwajima.

Kadhalika, alibainisha kwamba uvutaji tumbaku husababisha magonjwa ya moyo yakiwamo kiharusi, saratani, magonjwa ya njia ya hewa, mapafu na kisukari na ikiwamo yanayoathiri moyo, shinikizo la juu la damu na kifo cha ghafla.

Dk. Gwajima alisema siku hiyo huelimisha kuhusu madhara ya kiafya yatokanayo na matumizi ya bidhaa za tumbaku ikiwamo kuvuta, kunusa au kutafuna.

"Mtu anaweza kuepuka matumizi ya tumbaku na hivyo kuwa na dunia ya watu wasiotumia tumbaku kabisa. Ndiyo maana ujumbe wa mwaka huu unawasisitiza watu ambao wanatumia au wanaotaka kujaribu kudhamiria kuacha kabisa matumizi ya tumbaku na bidhaa zake ili kuilinda afya ya jamii nzima."

# Vyombo kusimamia taaluma habari mbioni

**Na Romana Mallya, DODOMA**

SERIKALI imesema inakamilisha mchakato wa uundaji wa vyombo vya kisheria vya kusimamia taaluma ya habari nchini, kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

Vyombo hivyo ni Bodi ya Ithibati na Baraza Huru la Habari, ambavyo kila kimoja kitakuwa na wajibu wake kwa mujibu wa sheria na kanuni, pamoja na kuhakikisha uwepo wa mfuko wa mafunzo kwa wanahabari.

Hayo yamesemwa jana bungeni na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo ya Sh. bilioni 54.7 kwa mwaka 2021/22, ambayo yalipitishwa na wabunge.

Alisema Bodi ya Ithibati itakuwa na jukumu la kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari wenye sifa, kusimamia maadili na nidhamu miongoni mwao.

Mengine ni kuishauri serikali kuhusu elimu ya kitaaluma na mafunzo ya wanahabari na kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni na maadili ya uandishi wa habari katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, Waziri Bashungwa alisema Baraza litaundwa baada ya bodi kuanza kazi, kwa kuwa litaundwa na wanahabari wenyewe watakaokuwa wamepewa ithibati.

Alisema pamoja na majukumu mengine, Baraza litakuwa linashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi kuhusiana na ukiukwaji wa maadili katika uandishi wa habari.

"Mfuko wa mafunzo kwa wanahabari utawezesha waandishi wa habari kupata mafunzo, kusaidia kuboresha na kuendeleza maudhui ya ndani pamoja na kufanyika kwa utafiti katika uandishi wa habari na mawasiliano ya umma," alisema.

Alisema sheria pia itatoa fursa ya kuwajengea uwezo wanahabari kimafunzo kupitia mfuko huo.

Vile vile, alisema sheria hiyo pia inawataka waajiri kuwakatia bima waandishi wa habari, lengo likiwa ni kuifanya taaluma ya habari kutambulika kisheria badala ya kila mtu kufanyakazi hiyo na kuweka misingi mizuri na kusimamia maadili ya taaluma ya habari.

Waziri Bashungwa alisema wigo wa vyombo vya habari umeendelea kuongezwa ili kuhakikisha wananchi kupata haki ya kikatiba ya kupata taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli zao.

Alisema katika kipindi cha mwezi Julai, mwaka 2020 hadi Mei mwaka huu, jumla ya magazeti na majarida mapya 14 yalipatiwa leseni na magazeti saba ni ya wamiliki binafsi na saba ni ya serikali.

Bashungwa alisema leseni 26 zilihuishwa zikihusisha leseni 25 za wamiliki binafsi na moja ya serikali.

"Hadi kufikia mwezi Mei, mwaka huu, Tanzania ilikuwa na magazeti na majarida yaliyosajiliwa 257 ambayo 206 yanamilikiwa na sekta binafsi, ikiwa ni sawa na asilimia 80.16 na 51 yanamilikiwa na serikali sawa na asilimia 19.84.

Waziri huyo alisema katika kipindi hicho, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni katika vituo saba vya redio, vyote vikiwa vinamilikiwa na watu binafsi, vituo vitano vya televisheni, vinne vinamilikiwa na watu binafsi na kimoja cha umma.

Alisema kwa upande wa maudhui mtandaoni, vituo 117 vya watoa huduma za televisheni kwa njia ya mtandao (Online TV) vilipewa leseni na vinne vya redio mtandaoni (Online Radio).

Pia alisema vituo 16 vya huduma za blogu mtandao ni pamoja na mtoa huduma mmoja wa Jukwaa Mtandaoni (Online forum) vilipatiwa leseni.

Waziri huyo alisema hadi kufikia mwezi Mei, mwaka huu, Tanzania ilikuwa na jumla ya vituo vya televisheni 43, vya halmashauri za wilaya ni vitatu, umma vitatu na vya binafsi 37.

"Kwa upande wa redio, kuna jumla ya vituo 200 ambapo vya halmashauri za wilaya ni vinne, vya umma viwili na vya binafsi 194. Televisheni mtandao ni 451, redio mtandaoni 23, blogu 122 na jukwaa mtandaoni tisa.

**"Hadi kufikia mwezi Mei, mwaka huu, Tanzania ilikuwa na magazeti na majarida yaliyosajiliwa 257 ambayo 206 yanamilikiwa na sekta binafsi, ikiwa ni sawa na asilimia 80.16 na 51 yanamilikiwa na serikali sawa na asilimia 19.84.**



Waziri wa Madini, Doto Biteko,

# Mkakati mpya kuhusu madini wanukia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema wizara hiyo imejipanga kuhakikisha inafikia malengo ya makusanyo kwa kuendelea kutekeleza mkakati wa kuhakikisha madini yote yanaongezewa thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma, Biteko alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 wamejiwekea malengo ya kukusanya Sh. bilioni 650 na kwamba watakahikisha kiasi hicho kinafikiwa mapema.

Alisema malengo hayo ni kutokana na kufanikiwa kwa asilimia 109.3 katika kukusanya mapato katika mwaka 2020/21 kwa kukusanya Sh. bilioni 527 hadi kufikia Mei, 2021 ikiwa ni mwezi mmoja kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha.

Katika kuhakikisha mkakati huo unatekelezwa, Waziri Biteko alisema tayari wizara imeshatoa leseni kwa mitambo mitatu ya kusafisha madini moja ni mkubwa uliyopo Mwanza wenye uwezo wa kusafisha madini yote ya dhahabu mwingine upo Geita na mmoja Dodoma.

Aliongeza kuwa pia wametoa leseni tano za mitambo ya kuchenjua madini kwa ajili ya dhahabu, shaba, nickel pamoja na Tin.

Aidha kwa upande wa madini ya vito, Waziri Biteko alisema kuwa wamefanya marekebisho ya sheria ya kodi na kuondoa kodi za kuagiza vifaa vya ukataji madini pamoja na kupunguza kodi ya madini yaliyokatwa ili kuwafanya wachimbaji kuingia kwenye ukataji zaidi.

Alisema jumla ya Lapidaries 467 za ukataji madini zimejengwa nchi nzima ambazo alisema zitasaidia kuleta teknolojia mpya ya ukataji madini pamoja na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Alisema baada ya muda Tanzania itashuhudia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na sekta ya madini kwani mitambo hiyo itatumika hata na wachimbaji wa nje kuja kusafisha madini hapa nchini.

Katika hatua nyingine Waziri Biteko, alisema serikali imejipanga vizuri katika ulinzi kuhakikisha hakuna madini yanayotoroshwa na kutoa wito kwa wachimbaji kuachana na tabia hiyo kwani wataishia jela au kuwa maskini endapo watabainika.


UBALOZI WA MAREKANI NA UINGEREZA DAR ES SALAAM

MNADA WA HADHARA

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani na Uingereza** watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani na Magari tarehe 5 June, 2021 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, China base, Hutch, Chest drawer, Dresser, Credenza, Dining table, Book case, Office desk, Chairs, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, electric cooker, A/c split units, Mashine za Photocopy , TV set, Computer set, Multifunction & Colour Printers na vingine vingi.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Toyota Land Cruiser Hard Top | 1HZ Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado TX | Diesel Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 2 | Ford Ranger Double Cabin | PF2H Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Hiace Min Bus | 5L Diesel Engine | 2008 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan URVAN Min Bus | ZD30 Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 2 | Suzuki Jimmy Station Wagon | M13 Petrol Engine | 2012/2014 | Haujalipwa |
| 1 | Land Rover Freelander 2 | SAL Petrol Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 2 | Ford Ecosport & Ford Figo | FY & YF Petrol Engine | 2012/2015 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 2 mpaka 4 Junne, 2021, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 10 June, 2021 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926 E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wachangamkie fursa ya kuondolewa vikwazo

JUZI serikali ilitoa tumaini jipya kwenye biashara mpakani kwa kufanikiwa kuondoa vikwazo 30 kati ya 64 vilivyoorodheshwa kukwaza biashara kati ya Tanzania na Kenya, huku yaliyobakia yakiwekewa mkakati maalum na muda wa utekelezaji.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, anataja yaliyotatuliwa kwa upande wa Tanzania ni pamoja na kuwezesha upitishaji wa bidhaa mpakani, hususan vinywaji baridi kama vile juisi kutoka nchini kwenda nchini humo.

Jingine ni kuondolewa kwa tozo za ukaguzi zilizokuwa zinatozwa na mamlaka za Kenya kwenye bidhaa za Tanzania, ikiwamo unga wa ngano kutoka nchini, kuwezesha kupitisha mahindi kwenda Kenya na kuondoa ushuru wa asilimia 25 kwenye bidhaa za kioo kutoka nchini kwenda nchini humo.

Mambo yaliyokubalika kwa upande wa Kenya ni upendeleo kwa bidhaa za saruji zenye ubora zinazozalishwa nchini humo, upendeleo maalum wa vinywaji kutoka Kenya ikiwamo juisi za nanasi na kuhakikisha bidhaa zinazoharibika mapema kama maziwa yanapovuka mpaka na kuingia nchini kwa kuzingatia taratibu za forodha.

Lingine ni kuongeza muda wa kibali cha kuingiza bidhaa za mifugo kutoka siku 15 hadi 30, huku wakiahidi kudumisha ushirikiano kwenye uchumi, biashara na uwekezaji, pamoja na kuunda timu ya maofisa wanne, ikiwa ni wawili kutoka kila nchi kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya mkutano huo.

Tunaipongeza serikali kwa kushughulikia vikwazo hivi kuwa sasa biashara baina ya nchi hizo itakwenda kufunguka na tutaona mabadiliko na ustawi ikiwa ni pamoja na nchi husika kupata kodi zitakazosaidia kuleta maendeleo kwa nchi zao.

Hii ni taarifa ya matumaini kwa wafanyabiashara na sekta binafsi kwa nchi zote, pamoja na Watanzania ambao wameajiriwa kwenye sekta hizo.

Ni wakati sasa wa biashara baina ya Tanzania na Kenya kushamiri kwa kuwa vikwazo vilivyokwaza vimeondolewa, sasa ni kwa namna gani wafanyabiashara wa nchi hizo watataumia fursa ili kujinufaisha wao, wananchi wenzao na kuchangia pato la taifa.

Kwa muda mrefu kumekuwa na fikra kuwa Wakenya wanachangamkia fursa zaidi ya Watanzania, na sasa tunataka kuona mabadiliko katika biashara kwa kuwa baadhi ya vikwazo vimepatiwa ufumbuzi.

Lakini ni muhimu pia kwa serikali kutatua vikwazo vya ndani ambavyo vinakwamisha ustawi wa wafanyabiashara nchini ili kuwawezesha kushindana, bila hivyo Tanzania itaendelea kuwa dampo la bidhaa kutoka nchi nyingine.

Ikiwa biashara baina ya nchi hizo itashamiri maana yake biashara za mazao na viwandani za Watanzania zitakuwa zimepata soko la uhakika na ajira zitaongezeka.


Lakini pamoja na mafanikio hayo ni muhimu kuchukua tahadhari kwamba sasa soko kama la maziwa lisijae bidhaa za nje huku za ndani zikishindwa kushindana, hasa kwenye bei, na lazima wafanyabiashara wetu wajengewe mazingira mazuri.

Tunatarajia jitihada zilizofanyika zitashuka hadi kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa ndani, ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

Kwa muda mrefu kuna kilio cha upatikanaji wa masoko na ukitembelea maduka mbalimbali utakuta maziwa yanayouzwa ni kutoka nje huku tuna wakulima wanaozalisha bidhaa hizo kwa wingi.

Kuondolewa kwa vikwazo hivi kuchukuliwe kama fursa ya ukuaji wa biashara, ajira na pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, na bidhaa za Tanzania zijulikane na kukubalika kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tumbaku isilindwe 'inachinja' mamilioni

KILA mwaka unapofika mwisho wa mwezi Mei ambao ulikuwa jana, dunia inajikumbusha kuacha matumizi ya tumbaku. Hivyo, kila Mei 31, wakulima wa tumbaku, wavuta sigara, ugoro, shisha au kuberi vinavyotengenezwa na zao hilo wanaambiwa kuwa kutumia tumbaku ni kifo.

Ni chanzo cha misiba inayotokana na saratani, maradhi ya moyo na figo na kwamba kila mwaka watu 8,000,000 duniani hupoteza maisha kutokana na sababu maradhi yanayoletwa na matumizi ya tumbaku.

Takwimu hizo zinazotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kuwa tumbaku ina madhara kiasi kwamba mataifa ikiwamo Tanzania yanatakiwa kuwajibika na kuachana nayo sasa.

Kwa Tanzania tumbaka hutumiwa zaidi kwenye kuvuta sigara zikiwamo za viwandani na sonyo zinazosokotwa kienyeji kwa kutumia makaratasi, pamoja na ugoro ambao zama hizi ni kilevi kinachotumiwa na vijana hasa mijini, kikiuzwa hadharani bila kificho na Wamasai bila kukatazwa kisheria.

Wakati wadau wanaendelea na kupinga matumizi ya tumbaku, ni wazi kuwa mamilioni ya Watanzania wanaathirika kutokana na wana familia kama baba, kaka, mjomba au rafiki yao kuvuta sigara nyumbani.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotangazwa na kipindi cha Kumepambazuka Radio One, jana, iwapo mwanafamilia anavuta tumbaku hasa sigara watu wengi wanaoishi naye wanaathirika. Ni kwa sababu moshi unaotoka unawafikia wengine wengi wanaomzunguka na kuathiriwa na kemikali ya 'nikotini'.

Lakini watoto kwa wakubwa wanadhurika kutokana na mabaki ya nikotini ambayo ni sumu yanayobaki kwenye makochi, viti, vitandani na mashuka wanayolalia, ukuta, na vifaa vingine vingi ndani ya nyumba, ikimaanisha kuwa wote ndani ya familia hawawezi kuwa salama.

Ni dhahiri kuwa watoto wanazaliwa kwa kulishwa kemikali ya 'nikotini', kwani kila mmoja anavutishwa sigara bila ridhaa yake na ndiyo maana WHO imeona athari za tumbaku na kusisitiza kupiga marufuku bidhaa zote za zao hilo.

**Tanzania bado serikali haijaanza kwa ukamilifu kampeni za kukataa tumbaku na mamilioni ya watu wako usingizini kwenye suala la kutumia bidhaa hizo zenye sumu inayoua.**

Tanzania bado serikali haijaanza kwa ukamilifu kampeni za kukataa tumbaku na mamilioni ya watu wako usingizini kwenye suala la kutumia bidhaa hizo zenye sumu inayoua.

Mathalani, Kumepambazuka inajadili namna baadhi ya wasanii wakubwa wanavyotangaza sigara, tena wale ambao wana wafuasi wengi na kuonyesha wasiwasi kuwa kitendo cha kuweka mabango ya kuwaonyesha wakivuta sigara ni jambo linaloweza kuathiri vijana na watoto wengi. Kwa ujumla serikali inashauriwa kupiga marufuku kwa sera, sheria na kimikakati.

Kumepambazuka Radio One, anawakumbusha wavutaji kuwa kuvuta shisha kwa saa moja ni sawa na kuvuta sigara kati ya 100 hadi 200 na kuwaonya kuwa wasivutike na shisha kwa vile imewekewa ladha ya kuondoa harufu ya tumbaku ila wafahamu kuwa mtu anapovuta kilevi hicho kwa saa moja ni hatari zaidi kwa sababu ni kama amevuta paketi tano au 10 kwa muda mfupi.

Jamii inakumbushwa kuwa tumbaku inaleta madhara kwenye mishipa ya damu na kusababisha isinyae na moyo kusukuma damu kwa nguvu sana, hata kuwa mkubwa na ndicho chanzo cha shinikizo la damu.

HABARI KITAIFA

# Ajinyonga hadi kufa madai kumfumania mchumba wake

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa Kijiji cha Mosufini wilayani Tunduru, Mohammed Said (22), amejinyonga hadi kufa huku akiacha ujumbe kuwa anatoa nafasi kwa mchumba aendeleze uhusiano na mwanaume aliyemfumania naye.

Taarifa zinaeleza kuwa Mohamed alichukua uamuzi huo jana saa 8:00 mchana baada ya madai ya kumfumania mchumba wake, Mwajuma Mtelela na mwanaume mwingine ambaye alikuwa rafiki yake, aliyetajwa kwa jina moja la Rasuli. Kwa mujibu wa taarifa hiyo Mohamed alijinyonga hadi kufa baada ya kutumia kamba kujifunga shingoni na kujining'iniza juu ya paa la chumba cha nyumba yao.

Akizungumzia tukio hilo, baba mzazi wa marehemu, Manoti Said, alisema baada ya tukio hilo waligundua kuwapo barua iliyoandikwa na marehemu kuwa amechukua uamuzi wa kujiua ili atoe nafasi kwa mchumba wake huyo aendeleze mahusiano yao (mchumba wake na mwanaume mwingine) bila kikwazo chake.

Alisema baada ya tukio hilo walitoa taarifa polisi ambao walifika eneo la tukio na kufanya taratibu za uchunguzi na baadaye kuwaruhusu wazike. Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Dk. Stephen Hokororo, alisema kuwa chanzo cha kifo chake kilitokana na kubana mfumo wa hewa na kusababisha kifo chake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na polisi wanaendelea na uchunguzi wa chanzo cha kifo hicho.



Mjasiriamali akiandaa kitoweo cha samaki katika Soko la Kimataifa la Samaki Feri, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Anayedaiwa jambazi sugu auawa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MTU anayedaiwa kuwa jambazi sugu, Iddi Masasi (43), ameuawa kwa kupigwa risasi wakati akijaribu kuwakimbia polisi waliokuwa wakimsaka kwa tuhuma za kufanya uhalifu wa kutumia silaha katika maeneo mbalimbali nchini.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa jana kwa vyombo habari, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa tano asubuhi katika soko la Nguzo Nane, mjini humo.

Alisema mtu huyo alikuwa akijihusisha na uhalifu katika Jiji la Dar es Salaam na baada ya kufanya tukio la unyang'anyi hivi karibu jijini humo, alikimbilia mkoani Shinyanga.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa kushirikiana kikosi kazi cha askari kutoka jijini Dar es Salaam, tulimsaka jambazi huyu na kumkuta maeneo ya Soko la Nguzo Nane," alisema Magiligimba.

"Baada ya kugundua anafuatiliwa na polisi alianza kuwakimbia, ndipo wakapiga risasi juu kwa ajili ya kumuonya, lakini aliendelea kukimbia ndipo wakampiga risasi kwenye mguu wa kushoto na mgongoni," aliongeza.

Alisema baada ya kujeruhiwa kwa risasi hizo alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, lakini alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu na mwili wake umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti hospitalini hapo.

Kamanda alisema mtu huyo mwaka 2011, alishawahi kufungwa jela miaka 30 katika Gereza la Butimba, jijini Mwanza kwa makosa ya unyang'anyi, lakini alitoka gerezani baada ya kukata rufani.

Katika hatua nyingine kamanda alitoa wito kwa wananchi mkoani Shinyanga, kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kutoa taarifa za uhalifu na kuwaonya majambazi kuacha kukimbilia mkoani humo.

# Magonjwa ya mlipuko yatishia wanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANAFUNZI 420 katika Shule ya Sekondari Nyengedi iliyoko Halmashauri ya Mtama Wilaya ya Lindi, wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo.

Nipashe lilifika katika shule hiyo na kukuta msururu wa wanafunzi wakisubiria kuingia katika vyoo vya shule hiyo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wanafunzi hao (majina yamehifadhiwa) walisema kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo wanalazimika kupanga foleni wanapohitaji kujisaidia wakati wa mapumziko.

Mbali na hilo, walieleza kuwa ili kuwahi kurejea darasani baada ya mapumziko, baadhi yao hulazimika kujisaidia vichakani, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa maisha yao na kuhatarisha kushambuliwa na wanyama wakali.

Wanafunzi hao walisema kitendo cha wao kujisaidia vichakani kumesababisha uchafuzi wa mazingira na usalama wa afya zao kuwa katika hatari kutokana na kuzuka magonjwa ya milipuko, kama vile kipindupindu na kuhara damu.

"Wakati wa mapumziko tunapohitaji kujisaidia tunalazimika tusubiriane kwa kusimama foleni wakati wa kuingia chooni, vinginevyo tunalazimika kujisaidia vichakani," walieleza wanafunzi hao.

Mkuu wa shule hiyo, Nuru Nabahani, alipofuatwa ili kueleza hali hiyo alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo, huku akitupia lawama wazazi na jamii kwa kutokuwa tayari kushiriki kazi za kujitolea licha ya kuwaomba wafanye hivyo.

"Sekondari yetu ina wanafunzi 420, wavulana 222 na 191 ni wasichana matundu ya vyoo yaliyopo sita tu, matatu wavulana na mawili walimu ambao idadi yao ni 12," alisema Nabahani.

Nabahani alisema kutokana na idadi ya wanafunzi waliopo wanahitaji angalau matundu ya vyoo kwa mgawanyo wa nane kwa wavulana na nane kwa wasichana.

Akizungumzia juu ya ushiriki wa wazazi na jamii katika jambo hilo, mkuu huyo alisema kitendo cha kutokuwa tayari kujitolea kunachangia uwapo wa upungufu huo, licha ya watoto wanaosoma ni wa kwao.

HABARI KITAIFA

# Makamanda Polisi kusimamia usajili kampuni za ulinzi kwa mfumo PSGP

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini limewahimiza wafanyakazi wote wa kampuni binafsi za ulinzi kuhakikisha wamesajiliwa kwenye kanzi data maalum kupitia Mfumo wa Kusimamia Sekta ya Ulinzi Binafsi Tanzania (PSG-P), likieleza kuwa sio suala la hiari.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Ulinzi Binafsi hivi karibuni jijini Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Isack Katamiti, alisema kuwa jeshi hilo litasimamia maelekezo hayo kupitia kwa makamanda wote wa mikoa ili kuhakikisha linatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

"Kuhusu PSGP, hii ndiyo habari ya mjini, haikwepeki hata kidogo. Na kuanzia sasa hivi tunaenda kuitolea maelekezo kwa makamanda wa polisi wa mikoa yote. Nimesema hivi makusudi kwa sababu ninazungumza na nchi nzima. Hapa hautakuwa na haja ya kuchanganya na za kwako, utapata maelekezo moja kwa moja kutoka kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wako," alisema ACP Katamiti.

ACP Katamiti aliongeza kuwa sekta ya ulinzi binafsi ina mambo mengi na inaajiri watu wengi kiasi kwamba hata serikali inapoteza kiasi kikubwa cha mapato endapo wafanyakazi wa kampuni binafsi za ulinzi hawatakuwa kwenye kanzi data hii maalum kupitia Mradi wa PSGP.

Kupitia mfumo huo, wafanyakazi wote wa sekta ya ulinzi binafsi husajiliwa kwenye kanzidata na kupewa namba ya utambulisho (Private Security Number - PSN) inatoyotolewa na Jeshi la Polisi kupitia mfumo huo wa PSG-P.

Alisema pamoja na kuhakikisha kuwa serikali haipotezi mapato yatokanayo na sekta hiyo, mfumo huo utasaidia Jeshi la Polisi kuratibu shughuli zote muhimu za sekta ya ulinzi binafsi kwa kuwa mfumo utawasajili wale tu wenye sifa na vigezo vya kutoa huduma za ulinzi kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo.

Awali, Dk. Shaban Kiwanga, Mkurugenzi wa TEHAMA wa Kampuni ya DataVision International iliyobobea katika masuala ya TEHAMA, ambayo inaratibu mradi wa PSG-P, alisema kwa kuzingatia kuwa wafanyakazi wa sekta ya ulinzi binafsi nchini wanakadiriwa kuwa zaidi ya 500,000 na uwapo wa kampuni za ulinzi takribani 2,000 nchini, ni lazima serikali iwe na nyenzo bora zaidi ya kupata taarifa na kuratibu shughuli za sekta hii kwa ufanisi na urahisi zaidi.

Alisema ingawa mradi huo umepitia changamoto nyingi hasa katika mwitikio wa wafanyakazi wa kampuni za ulinzi, lakini umefikia katika hatua nzuri ambapo idadi kubwa ya wafanyakazi wameshasajiliwa.

"Natoa wito kwa kampuni, ni lazima mlete taarifa zenu sahihi kwa ajili ya kuweka kwenye kanzidata. Kampuni imesajiliwa lini, ina wafanyakazi wangapi na watumishi ambao wanaongoza kampuni hiyo na maeneo ambayo wanalinda," alisema.

Naye Macmilan George, Mratibu wa Mradi wa PSGP, ilieleza kuwa wamezunguka katika mikoa mbalimbali nchini kwa lengo la kusajili wafanyakazi wa kampuni za ulinzi na bado wanaendelea na zoezi hilo.




Meneja wa Benki ya NMB wilayani Pangani mkoani Tanga, Abel Chitojo (kulia), akitoa maelezo ya uendeshaji wa benki hiyo kwa wateja wake juzi, katika mbio za Mwenge wa Uhuru wilayani Pangani Uwanja wa Bomani, benki hiyo imeanzisha bima ya mkono wa pole kwa wanakikundi kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Metropolitan, wengine ni wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM, PANGANI**

# Tisa wakamatwa tuhuma wizi wa lami

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

JESHI la Polisi mkoani Mtwara linawashikilia watu 25 kwa tuhuma mbalimbali, huku tisa kati yao wakishikiliwa kwa tuhuma za kuiba mapipa 60 ya lami yenye thamani ya shilingi milioni 15, mali ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Kamanda wa Polisi mkoani Mtwara, Mark Njera, alisema jana kuwa ukamataji huo ulifanyika kwa kipindi cha kati ya Mei 15 na 30, mwaka huu.

Alisema Mei 26 katika kituo cha Polisi Kati Mtwara kuliripotiwa wizi wa mapipa 60 ya lami yaliyofikishwa Mtwara na mkandarasi anayejenga barabara ya Mchinga na Uhuru katika Manispaa ya Lindi kwa lengo la kuchanganya lami hiyo na kokoto, uchanganyaji uliokuwa ufanyike kwenye mtambo maalum uliopo kampuni ya DB Shapriya.

"Mapipa yalipokewa na Hassan Mohamed Ally na kuyahifadhi katika eneo la Magengeni Mikindani, ili ayapeleke DB Shapriya, lakini yeye aliamua kuyauza," amesema ACP Njera.

Alisema katika operesheni hiyo walimkamata Hassan Mohamed Ally na wenzake wanane wakiwa na mapipa 32, huku msako wa kuwatafuta watuhumiwa wengine ukiendelea.

Katika matukio mengine, ACP Njera alisema jeshi hilo limefanikiwa kukamata TV moja aina ya Panasonic ya nchi 42, subwoofer moja aina ya sepiano na spika 4 zilizoripotiwa kuibwa katika eneo la Tandika Manispaa ya Mtwara. Vifaa vingine vilivyokamatwa ni maboksi manne ya vifaa tiba yakiwa na jumla ya paketi 200 za nyuzi ya kushonea binadamu na kumtaja aliyekamatwa ni Said David, mkazi wa Sinani Mtwara.

"Tukiwa tunaendelea na msako pia tulikamata vitu mbalimbali vinavyosadikiwa kuwa ni vya wizi ambavyo ni jiko moja la Oven, Subwoofer aina ya Seapeano ikiwa na spea zake, lakini tulishika pikipiki 2 aina ya TVS, pikipiki moja aina ya GSM na nyingine, waya wa fensi bando nne na Tv moja aina ya Aborder," alisema Njera.

## TAWA yatumia mabilioni kwa utalii wa vijijini

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetumia shilingi bilioni tisa kwenye vijiji na wilaya zinazonufaika na shughuli za utalii kwa maendeleo ya vijiji hivyo.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Misungwi, wakati akizungumza na waandishi wa habari ambapo alisema mamlaka hiyo imekuwa ikituma fedha kwa vijiji na wilaya zinazonufaika kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009.

Misungwi alisema fedha zote zilizotumwa kuanzia mwaka 2016/17 hadi kufikia mwaka 2019/20 kwenye vijiji kutokana na shughuli za utalii na shughuli za uwindaji wa kitalii.

"Wanavijiji wamekuwa wakipata fedha hizo zinazotokana na masuala ya utalii ikiwamo mgao wa kila mnyama ambao wao hupewa asilimia kadhaa," alisema.

Aidha alisema jumla ya wananchi 297,961 wamepatiwa elimu ya kuhifadhi mazingira pamoja na kujikinga na wanyama wakali na waharibifu.

Misungwi alisema wananchi wapatao 2,771 wametoka katika taasisi za elimu na vijiji 801 na wilaya 134 za Tanzania Bara.

HABARI KITAIFA

## OSHA yajikita kwa wajasiriamali wadogo

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), imezindua mpango maalum wa kuwasajili na kuwahudumia wajasiriamali wadogo.

Wajasiriamali watasajiliwa kupitia ukaguzi wa sehemu za kazi, kuwapa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kuhusiana na masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

Mpango huo umezinduliwa rasmi katika maonyesho ya wajasiriamali na wawekezaji yaliyohitimishwa mwishoni mwa wiki katika kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi mjini Kahama mkoani Shinyanga.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema mpango huo mahsusi umeandaliwa na taasisi yake baada ya kuendesha programu ya mafunzo kwa wajasiriamali wadogo kwa miaka mitano na kubainisha ombwe katika usimamizi wa usalama na afya miongoni mwa kundi hilo muhimu.

"Tumekuwa na programu ya mafunzo kwa wajasiriamali wadogo kwa zaidi ya miaka mitano, lakini hivi karibuni tulifanya tathmini ya mpango husika na tukabaini kwamba tunahitaji kuwa na utaratibu mzuri na rahisi zaidi kwa ajili ya kundi la wajasiriamali wadogo kukidhi viwango vya usalama na afya mahali pa kazi. Hivyo, tukaone tutengeneza mfumo wa kielektroniki utakaotuwezesha kuwasajili na kisha kuwafikia katika maeneo yao ili kuwaelimisha pamoja na kushauri namna bora ya kuboresha mazingira yao ya kazi," alisema Mwenda.

Mkurugenzi Mtendaji wa GS1 Tanzania ambao ndio waratibu wa maonyesho hayo kwa kushirikiana na kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi Kahama, Fatma Kange, alisema taasisi yake inashirikiana na OSHA katika kuwawezesha wajasiriamali kukuza biashara zao pamoja na kuwapa miongozo ya kuboresha mazingira yao ya kazi.

"Miaka 10 ijayo tunaanza kazi na OSHA na ndio maana unaona katika maonyesho haya OSHA amekuwa mdhamini muhimu sana kwa lengo la kuja kuelimisha wajasiriamali wetu ili wafanye uzalishaji kwa kuzingatia afya na usalama wao. Kama tunavyofahamu OSHA wana wajibu mkubwa wa kulinda rasilimali uhai na afya ya kila Mtanzania. Hivyo, tunataka wazalishaji wetu watambue nafasi ya afya katika shughuli zao za kila siku," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa GS1 Tanzania.

# 'Pedi zigaiwe bure kama zinavyotolewa kondom'

Na Yasmine Protace

KATIKA kusherehekea maadhimisho ya Siku ya Hedhi Duniani, wadau wameiomba serikali iondoe tozo katika taulo za kike ili ziweze kuingizwa nchini na kugaiwa bure kama kondom.

Mwenyekiti wa Kituo cha Maarifa na Taarifa, Selemani Bishagazi, alitoa ombi hilo katika maadhimisho hayo, yaliyoandaliwa na TGNP-Mtandao na kufanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari Msigani, mkoani Dar es Salaam.

Alisema kama kondom zinatolewa bure katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu, hata taulo za kike zitolewe bure kutokana na umuhimu wake.

Joyce Mkina kutoka TGNP-Mtandao alisema kuwa, taasisi hiyo ina imani kuwa nguvu ya pamoja itasaidia kupaza sauti na ushawishi kuondolewa kwa tozo kwenye bidhaa hiyo.

Alishauri kila shule kuwe na mpango wa kupewa bidhaa hiyo kwa ajili ya kumsaidia mtoto wa kike na pawapo na uwekezaji wa kiwanda cha kutengeneza pedi hizo kuleta ukombozi kwa wanawake.

Alisema matumizi mbadala ya pedi kama kutumia vitambaa kujistiri ni hatari kwa afya kwa sababu haijulikani vinahifadhiwa katika mazingira gani.

Naibu Meya wa Manispaa ya Ubungo, Hassan Silaji, aliwataka walimu wa shule za msingi na sekondari kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kujisitiri wanapokuwa kwenye hedhi.

Alisema anafahamu baadhi ya shule zinachangamoto ya matundu ya vyoo na maji.

"Hizo changamoto tutazimaliza kupitia fedha za bajeti zilizojengwa kwa ajili ya kutatua kero kwa watoto wa kike," alisema.

Aliwataka walimu kuwapatia elimu ya hedhi watoto wa jinsia zote ili waweze kujitambua.

Mwenyekiti wa Mtandao wa vituo vya maarifa na taarifa Ubungo, Neema Mwinyi, alisema katika kumkomboa mtoto wa kike inatakiwa kuwapo na bajeti ya mrengo wa kijinsia.

Alisema kuwa shule nyingi zinakabiliwa na ukosefu wa maji kwenye vyoo, ukosefu wa shimo la kuchomea taulo zilizotumika na vyumba vya kujistiri.




Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam (RCD), Nirmal Sheth (kushoto), pamoja na Mkurugenzi wa Miradi wa Klabu hiyo, Kumail Manji (wa pili kushoto), wakikabidhi moja ya madawati 140 kwa Diwani wa Kata ya Kinyerezi, Leah Mgitu, katika Shule ya Kinyerezi JICA, jijini Dar es Salaam juzi. Klabu hiyo na wadau wengine wametoa madawati 490 kwa ajili ya Shule za Msingi za Kinyerezi JICA, Kiyombo na Misitu ili kuboresha mazingira ya kujifunza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uzalishaji wa mbolea kuimarishwa

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya kimataifa ya mbolea Yara, imejipanga kuimarisha uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi, pamoja na kuingiza nyingine kutoka nje kwa ajili ya kukuzia mazao.

Akizungumza hivi karibuni na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mtendaji wa Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema lengo ni kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alisema kwa miaka 15 ambayo kampuni hiyo imekuwa ikitoa huduma hiyo nchini, imejikita zaidi katika kuwasaidia wakulima kwa kila namna.

Odhiambo alisema kampuni hiyo ina uwezo wa kuzalisha tani 10,000 za mbolea kwa mwaka na kwamba lengo ni kuimarisha uzalishaji huku kiasi kinachotoka nje ya nchi kikiwa tani 150,000.

Alisema mbali na kujiimarisha katika uzalishaji na uingizwaji wa mbolea bora inayolenga matakwa ya wakulima na afya ya udongo, kampuni hiyo inafanya kazi na vyama vya wakulima ili kuhakikisha wakulima wanapatiwa elimu zaidi ya kilimo hasa namna ya kufanya kilimo biashara.

Aidha, alisema lengo jingine ni kushirikiana pia na watendaji wa serikali kuanzia ngazi ya kata hata wilaya, mkoa na wizara kuwafikishia huduma wakulima.

Mkurugenzi huyo aliashauri wakulima kufanya kilimo cha kibiashara hasa kwa kuanzia kulima huku wakiwa wanajua pembejeo stahiki kutumia ikiwepo mbolea na faida nzima inayotokana na kilimo husika, jambo litakalosaidia wadogo kujikwamua kimaisha.

"Yara Tanzania inaungana na serikali katika kuwafikishia huduma na kuwaendeleza wakulima nchini hasa kwa kuwauzia bidhaa zinazotokana na uhitaji wa udongo wao na aina ya zao wanalolima," alisema.

Alisema Yara ina mbolea tofauti kulingana na uhitaji wa mkulima kwa zao na eneo analolima, program mahusus za mbolea zetu kwa ajili ya mazao kama mahindi, mpunga, kahawa, chai, tumbaku na mboga.

## Sifa ujumbe mabaraza ya ardhi zatajwa tatizo

BUNGE limeelezwa kuwa baadhi ya watu wenye madaraka ikiwamo wabunge, wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya, Kata na Vijiji hawana sifa za kuteuliwa kuwa wajumbe wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kalenga (CCM), Jackson Kiswaga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itawafanya wabunge kuwa wajumbe wa mabaraza hayo kutokana na ukweli kwamba migogoro mingi ya ardhi na mashamba hupelekewa kesi wao.

Akijibu swali hilo, Mabula alisema kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216, watu hao wenye madaraka hawana sifa za kuteuliwa.

"Lengo la kifungu hiki ni kuwezesha mgawanyo wa madaraka na utendaji kazi katika serikali, kwa kuwa wabunge ni wawakilishi wa wananchi wote katika maeneo yao endapo Mbunge atakuwa mjumbe wa Baraza la Ardhi," alisema.

Aidha, alisema wakati wa kutoa maoni ama maamuzi yanayompa ushindi mwananchi wa upande mmoja na kumnyima ushindi mwananchi wa upande wa pili suala hilo linaweza kusababisha malalamiko yanayohusu mgongano wa maslahi kutokana na nafasi zao.

"Wizara yangu inaendelea kutoa elimu kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Umma kwa ujumla kuhusiana na taratibu za utatuzi wa migogoro ya ardhi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

# Mkutano wa wadau kujadili alizeti

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuongoza mkutano mkubwa kuhusu mikakati ya uzalishaji wa zao la alizeti.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum, Nusrat Hanje.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kama Waziri yupo tayari kukutana na wakulima wa alizeti Mkoa wa Singida ili kuhakikisha wanalima kilimo chenye tija na kuondokana na kilimo cha desturi.

Bashe akijibu, alisema mkutano huo utafanyika mkoani Singida huu na utakutanisha wazalishaji na wakulima wa zao hilo.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kutumia mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora hususani za alizeti ambayo ndio zao la uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa wa Singida.

Akijibu swali, Bashe alisema serikali inatambua mchango wa alizeti katika kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula hapa nchini ambapo asilimia 68.9 ya mafuta ya kula yanatokana na zao hilo ikilinganishwa na mazao mengine ya mafuta kama vile michikichi, karanga, pamba, soya, nazi na ufuta ambayo huchangia asilimia 31.1 ya mafuta yanayozalishwa nchini.

Alisema serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za mafuta nchini kwa kutenga fedha Sh. bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ili kuzalishaji mbegu za alizeti na mbegu za mazao mengine kama mahindi, mpunga, michikichi, pamba, ngano, ufuta na mazao ya bustani.

Aidha, alisema lengo ni kuondokana na utaratibu wa mkulima na wazalishaji mbegu kwenda shambani kwa pamoja.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo kutawezesha kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti kutoka tani 538.71 msimu wa 2019/20 hadi kufikia tani 10,000 za mbegu bora za alizeti mwaka 2019/2030 ambazo zitatosha kutumika katika eneo la hekta 1,250,000 zinazoweza kuzalisha tani 500,000 za mafuta ya kula nchini.

"Katika kipindi cha miaka mitatu uzalishaji wa mbegu wa ASA umeendelea kuongezeka kutoka tani 74.2 mwaka 2016/17 hadi kufikia tani 166.0 mwaka 2019/20 na sekta binafsi ilizalisha tani 372.71," alisema.

Alisema kwa kuthamini umuhimu wa zao la alizeti, serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imeendelea kugundua na kuzalisha aina mpya ya mbegu bora za alizeti zenye sifa ya kutoa mavuno na mafuta mengi na zenye ukinzani dhidi ya magonjwa kutoka aina 1 hadi 17 za zao la alizeti msimu wa 2019/20.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Inocent Bashungwa, akiwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara hiyo ya mwaka 2021/2022 Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wastaafu wapewa siku 14 kuondoka nyumba za TBA

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Majengo (TBA), imetoa notisi ya wiki mbili kwa viongozi wa serikali na wabunge waliostaafu kupisha kwenye nyumba za TBA ili kutoa nafasi kwa viongozi waliopo madarakani kwasasa.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Mariam Ditopile.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani mahsusi wa kujenga nyumba za viongozi Dodoma kama ilivyofanyika Dar es salaam kwa kuwa Manaibu Waziri na Wabunge wamekuwa wakiomba kutafutiwa nyumba.

Akijibu, Waitara alikiri kuwa wabunge na viongozi wa serikali wamewasilisha maombi mbalimbali ya nyumba Dodoma.

"Kuna viongozi wengine walishastaafu ikiwamo wabunge na wengine sio tena viongozi wa serikali hadi sasa bado wanatumia hizi nyumba wameshapewa notisi, kwa hiyo ndani ya wiki mbili tunaamini baadhi ya wabunge na viongozi wa serikali watapata nyumba hizi," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa, alihoji kwanini serikali isijenge nyumba ambazo wataweka mkataba kwa wabunge kila baada ya miaka mitano ili kutoa nafasi kwa wabunge wanaoendelea na wapya.

Akijibu, Waitara alisema nyumba hizo zimekuwa na matumizi mabaya na wamebaini baadhi ya watu wanachukua nyumba hizo na kupangisha za kwao kutokana na kuwa na gharama nafuu.

"Tumeagiza TBA ipitie nchi nzima ikiwamo kuangalia madeni ya wadaiwa sugu ambao wameshindwa kulipa na kusababisha Wakala kushindwa kukarabati nyumba hizo."

"Kama kuna mtu alikuwa Mbunge na alichukua nyumba hapa Dodoma na amemaliza muda wake nyumba inapaswa kurejeshwa, na kama alikuwa kiongozi wa serikali nyumba inapaswa kurejeshwa ili itumike na viongozi wa wakati huo," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge Ditopile alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za Viongozi Waandamizi wa Serikali kama Makatibu Wakuu na Mawaziri katika Mji wa Dodoma kwa ajili ya makazi ya viongozi hao.

Waitara akijibu swali hilo, alisema tangu serikali kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Serikali Jijini Dodoma kumekuwapo na juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa viongozi waandamizi wa serikali wanapata makazi bora ya kudumu na yenye usalama.

"Katika kutekeleza hilo, serikali imeanza mkakati wa kujenga nyumba za viongozi katika Jiji la Dodoma, katika mwaka huu wa fedha 2020/21 Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imetenga kiasi cha Sh. bilioni 6 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 20 za viongozi na Sh. bilioni 4.0 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba 40 za viongozi jijini Dodoma," alisema.

Alisema hivi sasa kwa kutumia TBA hatua za ubunifu na usanifu wa nyumba hizo pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi zimekamilika.

Aidha, alisema ukarabati wa nyumba za viongozi jijini Dodoma unaendelea na katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba 20 za viongozi jijini humo na kuendelea na ukarabati wa nyumba nyingine 40 za viongozi zilizopo Dodoma katika maeneo ya Kisasa, Area 'D' na Kilimani.




Habari zote na Augusta Njoji

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 1, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Mambo kuvuta w/ulemavu kupenda shule ni haya hapa



Ukurasa 13

'Hakuna hedhi salama kwani mabinti wanafunzwa na dunia'

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# WILAYA YAPANIA KUTISHA KISAYANSI

■Yaja na shule maalum ya wavulana wanasayansi

HALMASHAURI ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, inajenga sekondari maalumu ya sayansi kwa lengo la kuhamasisha watoto kusoma michepuo ya sayansi ili kupata wataalamu mbalimbali kwenye fani hiyo.

Shule hiyo inayotarajiwa kuchukua wanafunzi 1,600 wa kidato cha kwanza hadi cha sita, ilianza kujengwa mwezi uliopita na kwamba kufikia mwishoni mwa mwezi (Juni 30) baadhi ya majengo yatakuwa yamekamilika, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Hassan Rugwa.

Anasema hadi ujenzi kukamilika, kazi hiyo inatarajia kugharimu Shilingi bilioni 3.5 mpaka nne na kwamba bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na nyingine zitatoka serikali kuu na michango kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu.

Mkurugenzi Mtendaji anasema katika mahojiano na Nipashe kuwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022, halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 516 zinazotokana na ushuru wa korosho kwa ajili ya ujenzi huo.

"Serikali imeahidi kutuchangia bilioni moja na wadau wa elimu wametuahidi kutupa chochote, kama mambo yatakwenda vizuri. Tunataka tukamilisha ujenzi wa miundombinu yote ya shule kwa miaka mitatu," anasema Rugwa.

Anaeleza kuwa shule itakuwa na madarasa 36, vyoo 24, mabweni 20 ya wanafunzi 1,600. Idadi ya wanafunzi ni 800 wa kidato cha kwanza hadi cha nne na wengine 800 ni wa kidato cha tano na sita.

"Katika shule hii, zitajengwa nyumba 42 za walimu, maabara mbili, maktaba, bwalo la chakula, zahanati, duka la 'min supermarket' na viwanja vya michezo ya aina mbalimbali," anasema Rugwa.



Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Hassan Rugwa, ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Ofisa Elimu Sekondari Andrew Muhulo, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Charles Mtabho na Katibu wa Afya wa wilaya hiyo, Geofrey Kombo, wakikagua ujenzi wa sekondari maalum ya wavulana. **PICHA: MTANDAO**

Anasema jitihada zinafanyika kuwaandaa walimu na watatoka maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi huyo anasema, halmashauri yake inataka shule hiyo iendane na kaulimbiu ya Tanzania ya kuwa na viwanda, kwa kuandaa wataalamu wa baadaye ambao ujuzi wao utatumika kusaidia kuifanya nchi kuwa ya viwanda.

"Nchi imedhamiria kuingia kwenye uchumi wa kati ambao ni wa viwanda, hivyo suala la sayansi haliwezi kuepukwa kwa sababu ni wakati wa kuwa na wataalamu wengi wa fani za sayansi," anasema.

Anasema, shule ya masomo ya sayansi inaweza kuisukuma Tanzania kuwa na wataalamu wengi wa baadaye wa fani mbalimbali, ambao watachangia kutosheleza mahitaji ya wataalamu katika sekta mbalimbali.

"Kutokana na uhaba wa wataalamu wa sayansi nchini kwenye maeneo mengi, wizara ilishaagiza kuwa wanafunzi wote wa elimu ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne wasome masomo hayo," anasema Rugwa.

Anasema, wakati wakiendelea na utaratibu huo ulioelekezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, wameona kuna haja ya kuwa na shule maalum ya masomo ya sayansi.

"Ili kuitikia wito huo wananchi wametoa maeneo yenye ukubwa wa ekari 60 kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo na baadhi yao wamechangia mifuko 500 ya saruji huku wadau wengine wakiwa wamekabidhi madawati 100 katika hatua za mwanzo," anasema.

**KUENDELEZA VIPAJI**

Ofisa Elimu Sekondari wa wilaya hiyo, Andrew Muhulo, anasema, kukamilika kwa shule hiyo kunatarajiwa kusaidia kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanafunzi ili viwe na manufaa kwa taifa.

"Vijana wengi wana vipaji, lakini ninaamini kwamba katika shule hii vitaibuliwa na kukuzwa zaidi ili viweze kuwanufaisha na pia kunufaisha taifa hapo baadaye," anasema Muhulo. Aidha, ofisa elimu huyo anasema hatua hiyo pia itasaidia kupunguza utoro ambao umekuwapo kwa wanafunzi wa kiume katika shule mbalimbali za sekondari wilayani Nachingwea na kufafanua kuwa, baadhi ya wanafunzi wa kiume wamekuwa wakijihusisha na biashara ndogo na shughuli nyingine ambazo haziendani na umri wao na hivyo kusababisha washindwe kuhudhuria masomo shuleni.

"Unafahamu, huku kwetu kuna utofauti na maeneo mengine ya nchi, ambayo wanafunzi wa kike ndiyo huwa ni watoro kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, lakini Nachingwea wanafunzi wa kiume wanaongoza kwa utoro," anasema.

Halikadhalika anasema, kwa vile shule itakuwa ni ya bweni, utoro wa aina hiyo unaweza kudhibitiwa kwa kuwa wanafunzi watakuwa wanaishi katika mazingira ya shule, hivyo hawataweza kuzurura.

"Tunaamini kwamba, kukamilika kwa shule yao maalum, kutasaidia kupunguza utoro huo, kwa kuwa watakuwa wanaishi shuleni kama ilivyo kwa wenzao wa shule ya sayansi ya wasichana ya Nachingwea Girls," anasema.

**KUBORESHA ELIMU**

Ofisa elimu huyo anasema, halmashauri imejiandaa kuwawezesha wanafunzi watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2022, wanaanza wote masomo kwa pamoja bila wengine kusubiri awamu ya pili. Anasema, Nachingwea ina shule 27 za sekondari ambazo 16 kati yake zina uhaba wa madawati 22, na kwamba wamepokea msaada wa mifuko 1,800 ya saruji kutoka kwa mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile.

"Mahitaji ni mfuko 1,320 ili kukamilisha ujenzi wa madarasa 22, mbunge ametoa mifuko 1,800, huu ni mwanzo mzuri, tutakamilisha ujenzi wa madarasa yote," anasema.

Anaeleza uhakika wake kuwa wapo wadau wengine wa elimu ambao wameahidi kuchangia kwa hali na mali katika ujenzi huo ili mwaka kesho usiwepo uhaba wa madarasa. Mbunge Dk. Chinguile anasema, hiyo ni awamu ya kwanza ya ugawaji wa saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kwa shule za sekondari jimboni mwake na kwamba ataendelea kuchangia zaidi.

"Ni wajibu wetu viongozi na wadau mbalimbali kuhakikisha tunashirikiana kuinua elimu katika wilaya yetu kwa kuboresha miundombinu ikiwamo ujenzi wa madarasa," anasema Dk. Chinguile.

Anasema, maendeleo ya Nachingwea yataletwa na watu wake wenyewe na kwamba hata wakipatikana wengine kutoka nje ya jimbo hilo, watataka kuona kwanza kile ambacho kimefanywa na wenyeji.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mambo kuvuta w/ulemavu kupenda shule ni haya hapa

JAMBO mojawapo linalowakatisha tamaa na hata kusababisha wanafunzi wenye ulemavu kuona shule si mahali pa kukimbilia ni miundombinu isiyojali hali ya wanaoishi na ulemavu iliyoko kwenye taasisi nyingi za elimu nchini.

Ukosefu wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu katika maeneo hayo ni moja ya changamoto zinazowakatisha tamaa watoto hao kuendelea na masomo kwa vile pamoja na kufuata elimu wanakumbana na shida zaidi wanapokuwa shuleni.

Baadhi ya shule zinatoa elimu kwa utaratibu wa elimu jumuishi kwa kuwafundisha wanafunzi mchanganyiko, walio na viungo timamu na wenye ulemavu. Hata huko, hakuna kuzingatia suala la miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, ikiwamo kujengwa njia maalum kwa ajili yao ili kuzifikia huduma zote zinazotolewa na zile zilizo mahususi kwa ajili yao.

Shuleni Buhangija katika Manispaa ya Shinyanya inatolewa elimu jumuishi inayowaweka pamoja wenye ulemavu wa kusikia, uoni hafifu, viungo na ulemavu mwingine mchanganyiko.

Buhangija ni miongoni mwa shule zinazojitahidi kutatua changamoto ya ukosefu wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.



Baadhi ya madarasa yenye miundombinu rafiki kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, Fatuma Jilala, anasema shule hiyo ina madarasa 23, lakini yenye miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu ni 16.

Anasema katika madarasa saba yaliyosalia kuwekewa miundombinu hiyo rafiki, yapo kwenye ukarabati ili kukamilisha mahitaji ya wenye ulemavu.

"Shule yetu ina jumla ya wanafunzi wote 1,049 na wenye ulemavu wapo 227. Muda wote tumekuwa tukijitahidi sana kuwaboreshea miundombinu ili iwe rafiki kwao," anasema Mwalimu Fatuma.

"Zamani shuleni hapa hatukuwa na miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, lakini kwa sasa mambo yamebadilika wanafunzi wanaingia darasani bila ya matatizo mengi, vifaa vya kuwafundishia vipo vya kutosha ikiwamo mashine ya kuchapisha maandishi ya nukta nundu kwa wasioona na wenye uoni hafifu," anaongeza.

Agnes Makambajeki mwenye uoni hafifu, ni mwalimu katika shule anayefundisha wanafunzi wenye tatizo kama lake, anasema shule inapokuwa na miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu inawapa ari ya kuipenda kusoma na kuhudhuria bila utoro.

Anaseme miundombinu inapokuwa rafiki, ni msaada kwa wanafunzi hao wenye ulemavu kwani wanaweza kujiongoza wenyewe kuingia darasani na hata kwenda msalani tofauti na ukosefu wa miundombinu hiyo ambayo huongeza kero na wengine kufikiria kuacha shule.

"Mimi pia nina tatizo la kuona, lakini kuwapo na miundombinu rafiki shuleni hapa nafarijika sana kuendelea kufundisha, pamoja na kuwapo na vifaa vya kutosha kufundishia wanafunzi hawa wenye mahitaji maalum," anasema Makambajeki.

Mwanafunzi mwenye uoni hafifu Modesta Daudi anayesoma darasa la nne shuleni hapo, anasema kipindi alipokuwa darasa la kwanza kabla ya shule kujengwa miundombinu rafiki kwao, alikuwa akipata shida kuingia darasani na msalani tena aliiona shule kama sehemu ya mateso.

Anasema uwepo wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu shuleni hapo, umempatia hamasa ya kupenda masomo zaidi, sababu hakuna matatizo kama zamani ikiwamo kuanguka wakati akipanda ngazi kuingia darasani.

"Tunaomba serikali iendelee kuboresha zaidi mazingira hapa shuleni, ili sisi wanafunzi wenye ulemavu tusipate shida katika masomo yetu, tufurahie kama wenzetu wasio na ulemavu, tusome na kutimiza ndoto zetu," anasema Modesta.

> "Shule yetu ina jumla ya wanafunzi wote 1,049 na wenye ulemavu wapo 227. Muda wote tumekuwa tukijitahidi sana kuwaboreshea miundombinu ili iwe rafiki kwao," anasema Mwalimu Fatuma.

Mwenyekiti wa Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA), Richard Mpongo, anasema suala la ujenzi wa mindombinu rafiki shuleni kwa wanafunzi wenye ulemavu upewe kipaumbele, ili kuondoa usumbufu shuleni.

Anasema shule ambayo haina miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, ni kikwazo kikubwa na usumbufu wa kupata elimu. Huwafanya wenye mahitaji kujiona kama wametengwa na wengine kukata tamaa ya kuendelea na masomo.

"Naiomba Wizara ya Elimu ilitilie mkazo suala hili la ujenzi wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu shuleni, pamoja na upatikanaji wa vifaa maalumu vya kuwafundishia na walimu wa kutosha wenye taaluma maalumu ili na sisi wenye ulemavu tuwe miongoni mwa wasomi wengi," anasema Mpongo.

Diwani wa Ibinzamata ilipo shule ya Buhangija, Ezekiel Sabo, anasema suala la kuwapo miundombinu rafiki kwenye madarasa yote shuleni hapo ni muhimu.

"Kila siku tumekuwa tukiipigia kelele manispaa kuyakarabati madarasa yaliyosalia kujengewe miundombinu hiyo rafiki kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu."

Anasema fedha zipo kwa ajili ya kujenga mindombinu rafiki katika shule hiyo, lakini anashangaa mpaka sasa ukarabati wa madarasa saba yaliyosalia kujengwa miundombinu hiyo, haujakamilika.

"Kama serikali imeahidi kuwatunza watoto hawa kwanini inashindwa kulimaliza ujenzi unaohitajika hili suala litamalizika lini au ni mpaka tupigiane kelele kila siku?" Anahoji Sabo.

"Naiomba halmashauri tuwajengee miundombinu rafiki hawa wanafunzi wenyewe ulemavu. Ni watoto wetu sote, tumalizie madarasa haya saba yaliyosalia ili wasome kwa furaha na kutimiza ndoto zao, tusiwe na mikwamokwamo isiyokwisha," anaongeza Sabo.

Ofisa Elimu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, anasema kazi ya ujenzi wa miundombinu inaendelea na kwamba kuna Shilingi milioni 15 zilizosalia wakati wa ujenzi wa madarasa mawili na uzio katika shule hiyo na ndicho kinachotumiwa kuendelea na kukamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

Anasema shule hiyo zamani haikuwa na miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, lakini leo ni miongoni mwa shule zinazothamini wanafunzi hao wenye mahitaji maalum.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# ‘Hakuna hedhi salama kwani mabinti wanafunzwa na dunia’

MASUALA ya hedhi pamoja na kujamiiana kwa mila na desturi za Tanzania ni mambo yasiyozungumzwa, au pale yanapotajwa ni kwa tahadhahari na kificho kikubwa. Ni kwa nadra wazazi, walezi na wanajamii kuongea masuala ya ngono, siku za mwezi na uhusiano wake na mimba za utotoni.

Ukimya huo husababisha wasichana kujulishwa habari hizo na watu wasio rasmi hatua ambayo ni kama kusema wanafundishwa kuhusu masuala hayo na ulimwengu ni mambo yanapoibuka wakati Nipashe inapozungumza na baadhi ya wanafunzi wa sekondari ya British ya jijini Dar es Salaam kuhusu maadhishimisho ya Siku ya Hedhi Salama Mei 27.

Wanasema wazazi, walezi, makabila mengi ya Tanzania na hata shule haziwaandai mabinti kwa ajili ya hedhi badala yake wengi husikia kwa marafiki, shuleni au watu wengine wakiwamo wanaume hasa kwenye masuala ya uhusiano.

Wanatahadharisha kuwa taifa haliwezi kuwa na hedhi salama kwa sababu mabinti wanafundishwa habari za siku za mwezi na dunia badala ya kufunzwa na mama, walezi wao.

Wanafunzi hao wanasema kwa vile suala la hedhi halizungumzwi limesababisha wasichana na watoto wengi zama hizi kuwa ‘wazazi’ na ‘walezi’ (wakiwa chini ya miaka 18 kabla ya kufikia umri wa utu uzima.

Dina Munisi anayesoma mwaka wa pili anawalaumu wazazi na walezi kwa sababu wanashindwa kuwapa wasichana taarifa za hedhi wanapoona wanakaribia kuingia kwenye hatua hiyo.

“Tuzungumzie kwanza kuhusu suala la kupevuka, mambo yanakuwaje, mabinti wafanye nini kuwa na hali salama katika kipindi hicho na ni vipi linachangia mimba za utotoni ili wasichana na wavulana wafahamu hali hiyo na kuepusha madhara ambayo tunayaona leo? Hedhi salama zitapatikana iwapo tutaanza kuvunja ukimya na kuwaelimisha watoto wetu.”

Anasema wasichana wengi wanaanza kudhalilishwa kingono wakiwa wadogo pengine wakiwa na chini ya miaka 10 na hata wanapofikia umri wa kupevuka kuanzia miaka 11, lakini wakati hayo yanatokea hawafahamu kikamilifu kuhusu ngono wala hedhi kwa sababu hawapati taarifa za mabadiliko kwenye miili yao.

“Tunasikia kwa wanaume, au wenzetu wengine. Kwa wanaume mara nyingi kama ametuona kuwa tunaelekea kufikia utu uzima wanaanza kuuliza kama tunaona siku zetu ndipo na kuanza kutupa taarifa hizo ambazo mara nyingi siyo kwa ukamilifu wakilenga kufundisha ujanja wa jinsi ya kuzuia kupata ujauzito lakini si kwa utaratibu unaowajenga wasichana.” Anasema Jane.

Anaungwa mkono na Jane Uledi, anayesema baadhi yao wanatoka vijijini kwenye shule ambazo hazina walimu wa kike wa kuwaeleza wasichana masuala kadhaa ikiwamo hedhi badala yake, shule zina walimu wanaume ambao huwakejeli mabinti kwa kuwapa majina ya kuwadhalilisha wanapozungumzia masuala ya hedhi.

Anatoa mfano kuwa binti anapoonekana amekuwa na mabadiliko na kuongezeka mwili utani unapoonza kutoka kwa walimu hasa wanaume. “Utasikia Jane vipi mbona umechokachoka au ‘Manchester inacheza,’ vitu vimeanza au mchezo wa Msimbazi,” anasema na kuongeza kuwa wasichana wengi hawafahamu anachomaanisha mwalimu na utani huo huisha bila wasichana kuelewa kinachoendelea.

Anasema hedhi hupewa majina mengi kwa mfano maeneo ya mijini kama ‘Man U’, ‘red dot’, masika, ‘reds’ na kwamba yapo mengine mengi yanayotumiwa vijijini na kwa ujumla hudhalilisha na kusababisha wasichana wasiwe na picha halisi wala taarifa za kuwaongoza kuhusu masuala ya hedhi.

Anashauri serikali kuangalia namna bora ya kupeleka walimu wa kike kila shule kwa ajili ya malezi, ulinzi na kusikiliza matatizo ya mabinti kuhusu kunyanyaswa kingono nyumbani, umri wa hedhi, athari za kuanza kujamiiana katika umri mdogo na taarifa sahihi za mambo yanayosababisha kupata mimba utotoni.



Mabinti wakifurahia kupata taulo za hedhi kwa uhakika na unafuu baada ya serikali kuondoa kodi kwenye bidhaa hiyo. **PICHA: MTANDAO**

> “Wasichana wengine hupelekwa kwa shangazi zao, bibi au watu wengine kuwafundisha masuala hayo, lakini leo hakuna sababu ya kufanya hivyo kwa kuwa mama au mlezi anaweza kumweleza binti mabadiliko na namna ya kumudu mihemko ya kingono.”

Akizungumzia suala hilo, Mwalimu Patrick Nolasco wa sekondari ya wasichana ya Kindoroko iliyoko wilayani Mwanga, anasema mama mzazi au mlezi ni mhusika mkuu wa kuzungumza na mabinti zake kuhusu masuala ya hedhi wakati wa walimu ni wa kike ni washirika katika kufanikisha hedhi salama.

“Ingawa hawa ndiyo wanaoaminiwa kuwa wa kwanza kuzungumza na mabinti kuhusu hali hiyo, hawazungumzi nao. Ni mila na taratibu zilizoko lakini zama hizi tunaamini kuwa kuna mabadiliko kinamama wa leo wameanza kuwafundisha mabinti badala ya kuacha wafundishwe na dunia.” Anasema Nolasco.

Anasema kuna baadhi ya mama wazazi au walezi wanaokaa kimya bila kuzungumza na wasichana kuhusu hedhi na inapotokea hasa pale ambapo msichana hakuwa na taarifa anaishia kupata taharuki, kuwa na hofu na kuchanganyikiwa jambo ambalo lisingetokea kama kungekuwa na mawasiliano.

“Wasichana wengine hupelekwa kwa shangazi zao, bibi au watu wengine kuwafundisha masuala hayo, lakini leo hakuna sababu ya kufanya hivyo kwa kuwa mama au mlezi anaweza kumweleza binti mabadiliko na namna ya kumudu mihemko ya kingono.”

Mhadhiri wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii (jina tunalo) Tanzania inahitaji kufanya utafiti wa kujua mbinu mbalimbali zinazofanyika katika makabila mengi kuwafundisha na kuwaandaa mabinti kuhusu taarifa za hedhi ili kuwa na hedhi salama.

Taasisi za elimu ya juu na watafiti wafanye utafiti kujua namna bora zinazofanywa na makabila mbalimbali kuwaelimisha na kuwaandaa wasichana kwenye hedhi na kuziboreshwa ili ikiwezekana zifundishwe kwenye mfumo rasmi wa elimu nchini kwa sababu kukosekana taarifa sahihi za wasichana kuanza siku za mwezi ndiyo mwanzo wa kuwa na mimba za utotoni shuleni na mitaani.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

### MREJESHO WA UWEKEZAJI...

# Kampuni SBL yaingiza vijana 71 vyuoni kusomea kilimo wakazalishe malighafi

## • Wote watokao familia 'hohehahe'




Mkurugenzi Mtendaji wa SBL Mark Ocitti (kulia) na Meneja wa Chuo cha Kilimo na Mifugo cha Kilacha Moshi, Padre Jerome Silayo (kushoto) na wanafunzi wa chuo hicho waliotembelea kiwanda cha SBL Moshi, ikiwa ni sehemu ya kujifunza kwa vitendo.
**PICHA: MAKTABA**

KILIMO hadi sasa ni sekta kubwa nchini na inachukua sura pana kuajiri, ndiyo sekta pekee sehemu kubwa ya Watanzania, huku katika pato la taifa likichangiwa zaidi ya robo.

Pia ndio sekta mchangiaji mkubwa katika upatikanaji wa malighafi ya viwandani, ambayo manufaa yake kimapato na matumizi yanafika mbali zaidi, kila kona.

Ikiwa ni sekta inayoajiri Watanzania wengi, takriban robo tatu au zaidi ya Watanzania na wastani wa theluthi mbili ya malighafi viwandani, kuna wakati katika uongozi uliopo, hata mamlaka za uongozi wa juu kitaifa iliainisha haja ya kuboreshwa sekta hiyo kwa maana ya tija katika sekta ya kilimo, inayoyumba.

Maana yake nini hapo? Ni haja ya kuwapo tija katika uzalishaji shambani. Na inapozungumziwa tija, maana yake ni ujuzi, elimu na hata vifaa zaidi shambani.

Hapo ina maana kilimo cha sasa kibadilike kuchukua mkondo huo hadi kufikia dira iliyoko kitaifa ndani ya miaka kadhaa ijayo, umwagiliaji uwe umechukua mkondo wa utekelezaji, ikienda sambamba na kushuhudiwa hekta zenye hesabu wastani wa milioni.

Hapo tena katika kufanikisha kuna suala la uwekezaji katika kufikia malengo hayo, ambayo inajumuisha utaalamu kutoka vituo vya utafiti wa kilimo (TARI), vilivyotapakaa sehemu mbalimbali nchini.

Pia vyuo vikongwe vya kilimo vya serikali vikishirikiana na visivyo vya kiserikali navyo vinashirikiana kubeba wataalamu, hali kadhalika kufanya ushauri wa kitaaluma, majukumu hayo yote yakipata mchango mkubwa kutoka kwab 'kigogo' wao Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA).

**UWEKEZAJI HURIA**

Inapozungumzia uwekezaji, ni mustakabali mpana unaobeba sura ya fursa huria, ambako kampuni binafsi katika kuwajibika kuweka mrejesho kwa umma, kuna suala lao la uwajibikaji maarufu 'corporate social responsibility'.

> Aina hiyo ya programu, inaendana na mahitaji ya sasa kuandaa Tanzania ya Viwanda katika upande wa mizizi ya sekta inayotoa malighafi, ikizingatiwa Tanzania sasa imeshapanda katika sakafu ya Uchumi wa Kati, ambao unaipa viwanda sura pana.

Kampuni mwekezaji huchagua eneo la kuweza ikishirikiana na umma au serikali kwamba ni mahali gani wanaweza kuwekeza katika hitaji la umma, ikiwa sehemu ya mrejesho wa faida kwa umma unakotumikia.

Hapo ndipo inapojitokeza simulizi ya Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), mzalishaji wa bia nchini na watumiaji wakubwa wa malighafi zinazotokana na kilimo, walipoamua kuweka mrejesho kwa wanaowazalishia malighafi; sekta ya kilimo.

Njia mojawapo ya kampuni hiyo imejikita katika kufadhili masomo ya wanafunzi wanaosoma kilimo kupitia programu inayojulikana kama 'Kilimo Viwanda.'

Hapo kukashuhudiwa jumla ya wanafunzi 71 waliolipiwa gharama zote za masomo katika vyuo vinne nchini, ambavyo ni: Kaole Wazazi kilichoko Bagamoyo mkoani Pwani; Mt. Maria Goretti, kilichopo mkoani Iringa; Chuo cha Kilimo na Mifugo cha Moshi, mkoani Kilimanjaro na Igabiro, kilichoko Muleba, Kagera.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL Mark Ocitti, ufadhili wa masomo unaotolewa na kampuni inalenga kuunga mkono jitihada za serikali kuongeza wataalamu wanaohitajika sana katika sekta ya kilimo.

Ocitti anasema ufadhili kupitia programu hiyo hutolewa kwa wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini, ambazo hazimudu magumu ya ada watoto wao.

Mkurugenzi huyo anasema wanufaika wa 'Kilimo Viwanda' pia wanapata fursa za kujifunza zaidi kwa vitendo kupitia programu za kuelekezwa na wataalamu mbalimbali, kupewa nafasi ya kujifunza kwa vitendo, kukitarajiwa itasaidia kuwaandaa vyema wawe wataalamu wenye weledi wa kutosha katika stadi yao.

Ocitti anajivuna kwamba kampuni yake ni mzalishaji mkubwa wa bia nchini anayetumia nafaka za ndani katika utengenezaji na hadi sasa wanafanya kazi na mtandao wa wakulima 400, ndani mikoa minane.

Anasema, kampuni yake inanunua nafaka aina ya shayiri, mahindi na mtama kwa ajili ya kuzalishaji bia, ikitumia wastani wa tani 17,000, ambayo ni sawa na asilimia 70 ya mahitaji SBL, huku malengo yajayo ni kufikisha asilimia 85 kufikia mwaka 2025.

Aina hiyo ya programu, inaendana na mahitaji ya sasa kuandaa Tanzania ya Viwanda katika upande wa mizizi ya sekta inayotoa malighafi, ikizingatiwa Tanzania sasa imeshapanda katika sakafu ya Uchumi wa Kati, ambao unaipa viwanda sura pana. Hali kadhalika, kilimo ambacho ni mzalishaji malighafi na chakula, nayo inakuwa tegemeo, hivyo wakiandaliwa vijana wanaotarajiwa kuwa maofisa kilimo wenye ujuzi na maarifa ya kutosha watakayoyatumia kuwasaidia wakulima kufanya kilimo chenye tija na hivyo kupata mazao mengi zaidi.

Wakati SBL ikionyesha mfano, ni safari inayohusu miradi yote iliyowekezwa na kampuni nyinginezo na hasa wadau katika sekta binafsi, kudumisha mkondo huo na wasioanza waanze kuzisaidia sekta hiyo katika safari kufikia Uchumi wa Kati na juu ya zaidi.



# Uzalishaji wa maziwa bado tatizo nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MSAJILI wa Bodi ya Maziwa Nchini, Dk. George Msalya, amesema Tanzania bado inakabiliwa na uzalishaji mdogo wa maziwa, huku kiasi cha Sh. bilioni 22 kikitumika kila mwaka kuagiza maziwa nje ya nchi.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya wiki ya maziwa ambayo hufanyika Juni mosi ya kila mwaka, kwa mwaka huu kitaifa yatafanyika jijini Tanga.

Alisema Tanzania inazalisha lita bilioni 3.4, ikigawanywa kwa idadi ya Watanzania, kila mtu atakunywa wastani wa lita 50 tu kwa mwaka wakati anapaswa kunywa lita 200.

"Kwa mujibu wa wataalamu wa afya mtu anatakiwa kunywa maziwa lita 200 kwa mwaka, hivyo bado kuna uhitaji mkubwa wa uzalishaji zaidi wa maziwa ni kinywaji muhimu kwa afya ya binadamu," alisema.

Hata hivyo, alisema bado uelewa ni mdogo kwa watu badala ya kunywa maziwa wanakwenda baa kunywa pombe wakati maziwa ni muhimu kuliko pombe.

"Tangu kuanzishwa kwa bodi hii mwaka 2005 Tanzania imepiga hatua katika uzalishaji wa maziwa, ambapo hadi mwaka 2015 kila mtu alikuwa anakunywa lita 40 hadi 45,"alisema.

Alisema hadi kufikia mwaka 2021 kila mtu anakunywa maziwa lita 50 kwa mwaka, katika pato la Taifa maziwa yanachangia kwa asilimia 30 huku katika sekta ya mifugo ikichangia kwa asilimia saba.

Dk. Msalya aliwataka Watanzania kuwa na uzalendo wa kutumia bidhaa za ndani za maziwa ili kuwainua wafugaji, wasindikaji na wachakataji wa bidhaa hiyo kwa kuwa zipo bidhaa nzuri za maziwa zinazotengenezwa nchini.

Aidha, alisema katika maadhimisho hayo yatalenga katika kufanya utafiti kuhusu tasnia ya maziwa, kujifunza namna ya kufuga ng'ombe bora wa maziwa na kugawa maziwa kwenye makundi mbalimbali ikiwamo wagonjwa waliopo hospitalini.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akipokea maelezo kutoka kwa Meneja wa TANESCO mkoani humo, Mhandisi Kenneth Boimanda, alipotembelea banda la TANESCO katika maonyesho ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi yanayoendelea katika Uwanja wa Jamhuri jijini humo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Ujenzi kituo jumuishi cha utoaji haki wafikia 85%

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UJENZI wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC), umefikia asilimia 85 ambapo utasaidia kurahisisha utoaji huduma za haki kwa wananchi.

Kituo hicho kinajengwa na mkandarasi Hainan International LTD utekelezaji wake ulianza Januari 22, mwaka jana, hadi kukamilika utagharimu Sh. bilioni 9.2.

Mhandisi wa Mahakama ya Tanzania, Fabian Kwagilwa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akikagua ujenzi wake ukiwa ni utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitano wa Mahakama.

Mhandisi Kwagio alisema ujenzi wa kituo hicho umezingatia mambo muhimu kadhaa kwa ajili ya usalama wa watu watakaoingia kupata huduma zakihaki pamoja na watoaji huduma za haki kimahakama.

Aliyataja mambo ambayo yamezingatiwa ni pamoja mazingira bora ya kisasa na rafiki katika utekelezaji wa shughuli za kimahakama, ikiwamo mifumo mbalimbali inayotumia teknolojia yakisasa.

Kwa upande wake, Mtendaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Maria Itala, alisema mkoa huo ni moja ya mkoa kati ya mitano ambayo imebahatika kupata kituo kama hicho na kwamba jengo litajumuisha ngazi zote za Mahakama katika utoaji huduma za Mahakama ya Mwanzo, Wilaya, Hakimu Mkazi pamoja na Mahakama Kuu.

Alisema jamii itakayokuja kupata huduma za utoaji haki ambazo zitaendeshwa kwa teknolojia ya kisasa huduma zote zitapatikana hapo na kuepusha usumbufu wa mtu kutoka mahakama moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta haki.

# Jamii yahimizwa kulima mchicha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa jukwaa la ubunifu la mchicha wameihamasisha jamii kuongeza uzalishaji wa mchicha ili kujikwamua kiuchumi na kuimarisha lishe bora.

Jukwaa hilo lilikutana jijini hapa kwa lengo la kupata uelewa wa uzalishaji, usindikaji na matumizi ya zao la mchicha.

Akizungumza katika kikao cha jukwaa hilo, mmoja wa wakulima, Jane Mabwai, alisema kwa sasa kuna aina tatu za mbegu za mchicha ambazo ni Poli, Akeri na Nguruma ambazo zitasaidia jamii katika kilimo cha biashara na lishe bora.

Alisema mbegu hizo ni bora kwa kuwa zinazalishwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na zinastawi kwa muda mfupi, hazishambuliwi na magonjwa na zinaimarisha afya za walaji.

Mkulima huyo alisema aina hizo za mchicha zitawaongezea kipato kutokana na kutoa mavuno mengi ukilinganisha ya ile ya kienyeji waliyokuwa wakitumia awali.

Awali, Mratibu wa mradi wa mchicha wa kushangaza Emmanuel Laswai, kutoka Kituo TARI Tengeru, alisema mbegu hizo zina protini zaidi ya nyama kwa asilimia 15.

Alisema mchicha huo unastawi kwa siku 21 na unavunwa kwa miezi mitau na kuwataka watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya mbegu zilizofanyiwa tafiti ili kujikwamua kiuchumi.

Laswai, alisema mradi huo wa mchicha wa kushangaza unatekelezwa katika maeneo mbalimbali kupitia kanda zake zote na unafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la GIZ.

"Vijana sio lazima kuendesha bodaboda vijana walioko mtaani wanaweza kutumia kilimo hichi kijipatia kipato kwa muda mfupi kwani sifa nyingine iliyopo katika mchicha huu ni kutosumbuliwa na magonjwa," alisema.

Mratibu huyo, aliongeza kuwa mchicha huo ni muhimu kwa matumizi ya lishe ya watoto wadogo kutokana na kuwa na uwezo mkubwa wa kuimarisha afya zao.

"Ili kuondokana na tatizo la udumavu nchini mchicha huu utakuwa msaada mkubwa kutokana na kuwa na madini mengi pamoja na protini muhimu katika ukuaji wa afya za watoto," alisema Laswai.

Naye Meneja wa TARI Tengeru, Dk. Mpoki Shimwela, alisema kuwa lengo la jukwaa hilo ni kuwezesha wakulima kupata teknolojia mbalimbali zinazofanyiwa utafiti katika kilimo cha mchicha.

"Tumekuwa na majukwaa kama haya katika kanda tano za TARI nchini, lengo ni kuhamasisha wakulima kutumia mbegu hizi za mchicha ili kujikwamua kiuchumi lakini pia kuimarisha afya za watumiaji," alisema Dk. Shimwela.

Alisema ili kusaidia kupatikana kwa soko la uhakika wa kilimo hicho wanaiomba serikali kutengeneza sheria ndogo, ambazo zitalazimisha watengenezaji wa unga wa lishe wa watoto kutumia mchicha huo kuongeza virutubisho lishe.

Alibainisha kuwa sheria hiyo itasaidia kuimarisha na kulinda afya ya watoto pamoja na kuondokana na tatizo la udumavu na watoto wasiofundishika darasani.



# Wanaushirika wanufaika na bima ya afya CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) zimeendelea na utekelezaji wa mpango wa "Ushirika Afya" kwa kuingia makubaliano na Chama Kikuu cha Ushirika cha Maziwa mkoani Tanga kwa ajili ya kuwapatia bima ya afya wanachama wake.

Kutokana na hatua hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, ameipongeza Benki ya CRDB na NHIF kwa ubunifu wa mpango huo ambao utawafaidisha wakulima wengi nchini.

"Nasihi wanaushirika katika Mkoa wa Tanga kutumia fursa hii tujiunge kwa wingi kwenye vyama vya ushirika ili kutumia fursa hii kuboresha maisha ya familia zetu," alisema Mwilapwa.

Ofisa Biashara Mkuu wa CRDB, Dk. Joseph Witts, alisema katika makubaliano hayo Benki ya CRDB itawawezesha wanachama wa chama kikuu kulipia bima ya afya bila riba yoyote, hivyo kuboresha uzalishaji wa maziwa katika Mkoa wa Tanga.

"Huu ni mpango maalumu wa benki yetu unaolenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya katika maisha ya wateja wetu walioko kwenye sekta ya kilimo nchini kote," alieleza Dk. Witts.

Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa NHIF, Christopher Mapunda, alisema NHIF katika mkakati huu inalenga kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wakulima na wafugaji nchini.

"Mpango utawawezesha wazalishaji wa maziwa kupata huduma za afya katika vituo zaidi ya 8,000 katika nchi nzima," alieleza Mapunda.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa mkoani Tanga, Shamte Said, aliwashukuru Benki ya CRDB na NHIF kwa kuja na mpango huo. "Nawapongeza kwa kuwakumbuka wazalishaji wa maziwa nawaahidi tutatumia fursa hii kujihakikishia upatikanaji wa matibabu," alisema Shamte.

Hafla ya utiaji sahihi wa makubaliano hayo ilihudhuriwa na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Tanga, Maofisa wa NHIF, Maofisa wa Benki ya CRDB na wajumbe wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Maziwa Tanga.

# Viongozi wa kijiji matatani kwa madai kuachia watuhumiwa uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameamuru Jeshi la Polisi kuwasweka ndani viongozi wanne wa Kijiji cha Mlima Njiwa Kata ya Mbungani wilayani Chunya kwa tuhuma za kuwaachia watuhumiwa wa uhalifu katika mazingira yenye utata.

Viongozi ambao Homera aliagiza wakamatwe ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Grace Luanda, Mwenyekiti wa Kijiji hicho, George Ndowolo pamoja na wajumbe wawili wa Serikali ya Kijiji ambao ni Bahati Mwaijande na Isack Mgogo huku akiagiza jeshi hilo kumsaka Steven Mtakuzi ambaye hakuwapo kwenye mkutano.

Alitoa amri hiyo mwishoni mwa wiki wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipofika katika kijiji hicho kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi na kutatua migogoro baina ya wachimbaji wa madini katika kijiji hicho.

Kabla ya kutoa amri hiyo, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliibua kero hiyo wakidai kuwa waliwakamata wezi waliokuwa wanawaibia nguo zao na kuwapeleka kijijini hapo na kuwapeleka kwenye ofisi ya kijiji ili wachukuliwe hatua lakini viongozi hao wakawatosa.

Mmoja wa wananchi hao, Daniel Mwashambwa, alisema waliwakamata watu hao ambao walikuwa wanawake wawili na kuwahifadhi kwenye ofisi ya kijiji, lakini kesho yake wanaenda wakakuta wahalifu hao hawapo.

Alisema walipowahoji viongozi hao walijibiwa kwamba watuhumiwa hao walikuwa wameshapelekwa katika Kituo cha Polisi Chunya, lakini wakawa na wasiwasi.

Alisema ili kujiridhisha kwamba watuhumiwa hao walifikishwa polisi, waliamua kupiga simu na wakaambiwa kwamba watuhumiwa hao walikuwa hawapo na hawakuwahi kufikishwa.

"Tungejichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wezi wale tungekuwa tayari tupo ndani, sasa hawa viongozi waliwatorosha na tuna wasiwasi yawezekana waliwapatia rushwa, tunaomba Mkuu wa Mkoa utusaidie," alisema Mwashambwa.

Naye Lesta Mwafongo alisema viongozi hao wa kijiji walizichukua nguo ambazo watuhumiwa walikutwa nazo wakawagawia waliokuwa wameibiwa badala ya kuzipeleka polisi kama ushahidi.

Hata hivyo alisema baadhi ya nguo walizowakuta nazo watuhumiwa hao zimepotea katika mazingira ya kutatanisha na kila wakifuatilia hawazioni na watuhumiwa hawapo kijijini wala Polisi lakini walipopeleleza waliambiwa kuwa walirudi kwao Sumbawanga mkoani Rukwa.

Baada ya maelezo hayo ya wananchi, Homera alimhoji Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo ili kujua kama kweli watuhumiwa hao walifikishwa kituoni na akajibiwa kuwa hawajawahi kufikishwa.

Kutokana na majibu hayo, Homera aliamuru Jeshi la Polisi kuwakamata viongozi hao na kuwasweka ndani ili wahojiwe kuhusu utaratibu uliotumika kuwaachia watuhumiwa hao.

"Hawa wakamatwe na wapelekwe kituoni ili wakahojiwe na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), maelezo haya yanaashiria harufu ya rushwa, wanatakiwa wakajieleze huko," alisema Homera.

Alisema lengo la kuwasweka ndani viongozi hao ni kukumbushana mipaka ya kazi na wala hakulenga kumkomoa mtu, huku akiwataka wananchi kuendelea kushirikiana na viongozi wa vijiji kutokomeza uhalifu.



Mtafiti wa zao la ulezi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, Dennis Tippe, akitoa maelekezo namna bora ya kulima zao hilo kwenye moja ya mashamba darasa yaliyopo kwenye kituo hicho juzi, wakati wa maonyesho ya kilimo biashara yaliyofanyika jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Serikali yaagiza kupima afya ya udongo nchi nzima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeanza kupima afya ya udongo nchi nzima, kwa lengo la kuandaa ramani maalum itakayoonyesha maeneo ambayo mazao ya aina mbalimbali yanaweza kustawi na kiwango cha mbolea kinachohitajika ili kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija.

Mradi wa kupima afya ya udongo nchini unafanywa na kampuni ya OCP kwa niaba ya serikali na kwa kuanzia utatekelezwa katika mikoa minne ya Morogoro, Rukwa, Mbeya na Iringa.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya OCP, Dk. Mshindo Msolla, alisema wameamua kuanzisha mkakati huo ikiwa ni jithada za kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija na kupata faida kupitia kilimo.

Alisema maeneo mengi nchini wakulima hawana elimu juu ya aina gani ya udongo inafaa kulimwa zao gani matokeo yake hulima mazao yoyote na kuingia hasara.

"Baada ya kubaini tatizo kwenye afya ya udongo, kampuni yetu imekuja na suluhisho la kudumu kupima afya ya udongo ili sasa kila mkulima katika eneo lake atambue aina ya zao atakalolima kwa kuzingatia matumizi ya mbegu bora, mbolea na wataalamu," alisema Dk. Msola.

Alisema maandalizi ya kuanza zoezi la upimaji afya ya udongo limekamilika, na kwamba wataanza kufanya kazi kwenye mikoa hiyo minne na malengo yao ni kufikia mikoa yote Tanzania ili kuwasaidia wakulima kupata faida katika kilimo kuliko ilivyo sasa ambapo wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Uyole mkoani Mbeya, alisema wamepewa jukumu la kutekeleza mradi huo wa upimaji afya ya udongo kwenye mikoa minne.

Alisema kwa kuwa wao ni watafiti wa kilimo, wanauzoefu hivyo watakwenda kumaliza kabisa tatizo la afya ya udongo kwenye maeneo mbalimbali ya mradi.

Alisema licha ya kuanza zoezi la upimaji wa afya ya udongo, lakini TARI wanaendelea kuwafundisha wakulima matumizi bora ya ardhi, teknolojia za kisasa na kuwapatia wataalamu wa kilimo ili kufundishwa namna bora ya kuzalisha mazao yao.

Mkuu wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Kalorius Misungwi, aliwapongeza wadau hao kwa kuanzisha mradi ya upimaji afya ya udongo kwa madai kuwa kulikuwa na tatizo kubwa ya virutubisho vya udongo hali iliyosababisha wakulima kupata hasara kwenye mazao yao.

Alisema mradi huo utasaidia wakulima kujua aina za mbegu, mbolea zinazopaswa kutumia kulingana na eneo pindi msimu wa kilimo unapowadia.

# 'Viongozi msiokuwa madarakani tokeni kwenye nyumba za umma'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi, Maendeleo na Makazi, Riziki Pembe Juma, amewataka waliokuwa viongozi wa serikali ambao wameshapoteza sifa kuhama katika nyumba za serikali ili kutoa nafasi kwa wenzao walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali kuishi katika nyumba hizo.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hotuba ya makadirio na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika kikao cha baraza hilo kinachoendelea Chukwani.

Riziki alikiri kuwa ni kweli wapo baadhi ya watu ambao wameshapoteza sifa ya kuwa viongozi lakini wameng'ang'ania kuishi katika nyumba hizo hivyo ni vyema kuhama mara moja.

Alisema kuwa kuna nyumba 84 zilizoko Unguja zikiwamo 32 kwa ajili ya kukaa viongozi mbalimbali wa serikali ambapo nyumba hizo mwaka 2018 zilikabidhiwa Wakala wa Majengo Zanzibar.

Alieleza kuwa nyumba hizo baadhi zimechakaa na zinahitaji matengenezo ili kwenda na hadhi ya viongozi kwa vile zimeshakaa na zinahitaji matengenezo makubwa.

Aidha, alisema wizara anayoiongoza itahakikisha inaliendeleza Shirika la Nyumba Zanzibar ili kujenga nyumba mpya za makazi na kukidhi mahitaji ya wananchi.

Akichangia bajeti hiyo mwakilishi wa viti maalum, Mgeni Hassan Juma, alisema kuwa nyumba za maendeleo ambazo zimejengwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume ni kwa ajili ya wanyonge si kwa viongozi.

Alisema inasikitisha kuona kuwa nyumba hizo hivi sasa zimevamiwa na viongozi na wananchi wanyonge wanateseka kwa kukosa nyumba na mahali pa kuishi.

"Viongozi wengi wamejichukulia nyumba za Michezani, matokeo yake wanyonge wanakosa nyumba za kuishi ni kwa sababu gani wakati lengo halikuwa hivyo hapo awali?" Alihoji.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Welezo, Hassan Khamis Hafidh, aliitaka serikali kusimamia usimamizi wa ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi na ujengaji holela.



Waathirika mbalimbali wa uwekezaji katika kampuni ya Masterlife wakifuatilia kwa makini kikao cha kamati kilichofanyika ukumbi wa Taqwa Mlandege Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ripoti ya mkaguzi wa hesabu kutinga barazani wakati wowote

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametakiwa kujiandaa na kuichangia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2019-2020 ambayo inatarajiwa kuwasilishwa barazani hapo wakati wowote kuanzia sasa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Professa Omar Fakih Hamad, aliyetaka kujua lini ripoti hiyo itawasilishwa barazani hapo.

Waziri huyo aliwaambia itawasilishwa kwa ajili ya kukidhi matakwa ya kikatiba na sheria ambayo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watapata nafasi ya kuichangia na kutoa maoni yao.

Aidha, aliwataka wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (PAC), kujipanga na kuisikiliza kwa makini ripoti hiyo.

"Mheshimiwa Spika nataka kuchukuwa nafasi hii kuwajulisha wajumbe kujitayarisha na kujipanga kwa ajili ya kuichangia ripoti ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali ambayo tayari imewasilishwa na kukabidhiwa Rais," alisema.

Waziri huyo alisema kwa mara ya kwanza ripoti hiyo iliwasilishwa hadharani mbele ya Rais ikiwa ni sehemu ya kujenga uwazi katika misingi ya utawala bora.

Alitoa ufafanuzi huo baada ya mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Ussi kuuliza kwa nini ripoti hiyo ilisomwa hadharani na haoni kujitokeza kwa athari kwa watu waliotajwa waziwazi kuwa wana tuhuma.

"Mheshimiwa Spika hizi ni zama za uwazi hakuna la kuficha ni vizuri taarifa kama ile muhimu kuweza kutangazwa hadharani na wananchi kufahamu kinachofanyika," alisema.

Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, wiki iliyopita alipokea ripoti ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali kwa mwaka wa fedha 2019-2020 ambayo imeibuwa taarifa mbalimbali za matumizi mabaya ya fedha katika mashirika ya umma na taasisi zake.

## Wakumbushwa kupima afya zao mara kwa mara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais, Zuhura Kassim Ali, amewataka wananchi kuwa na utaratibu wa kuchunguza afya zao pale wanaposikia kuna fursa za kuhudumiwa na wataalamu, kabla ya maradhi kujitokeza ili kuwa na namna bora ya kuyatibu.

Akizungumza baada ya kupatiwa matibabu na madaktari wa Jumuiya ya Zanzibar Outreach Program (ZOP), matibabu ambayo yaliandaliwa na Shule ya Madrasatul Ahabaab ya Kisauni kwa ushirikiano na ZOP yaliyofanyika Kisauni mjini Unguja.

Alisema, afya ndiyo kila kitu kwa binadamu hivyo ni vyema wananchi kuwa na utaratibu wa kwenda kuchunguzwa kwani siha ni rasilimali muhimu katika maisha ya binadamu.

Aidha, alisema baadhi ya wananchi hawana utaratibu wa kuangalia afya zao hadi litakapotokezea tatizo jambo ambalo halifai kwa binadamu kwa vile kinga ni bora kuliko kutibu na inakuwa changamoto zaidi wanapopata magonjwa makubwa.

"Kwa kweli mimi nimepimwa na nimefurahi na nashukuru sikuwa na tatizo lakini nimefurahi wenzangu waliangaliwa afya zao na waliogundulika na tatizo wamepata ushauri, nasafa na kupatiwa matibabu" alisema.

Aidha, alisema kumekuwapo na baadhi ya wagonjwa waliochunguzwa na kubainika kuwa na ugonjwa ambayo wenyewe walikuwa hawayajui matatizo yao, hivyo aliwasihi wananchi kuwa na tabia ya kuangalia afya zao mara kwa mara.

Aliwashauri wananchi wanaposikia zoezi la matibabu linapofanyika sehemu yoyote kujitokeza kwa wingi kwenda kufuata matibabu ili kujua matatizo yanayowakabili na kuacha ugonjwa ufike hatua ya kuwa mkubwa.

Mwenyekiti wa Zanzibar Outreach Programu , Walid Kassim Mohammed, alisema, katika kambi hiyo mwitikio wa wananchi ulikuwa mkubwa na wamewapatia matibabu wanafunzi na wazazi wao pamoja na wananchi waliofika katika kambi hiyo ya tiba.

Alisema kambi hiyo imekuwa ikiimarika kila mwaka na hapo awali walikuwa wakiwapa matibabu wanafunzi na walimu wa Shule ya Madrasatul Ahabaab ya Kisauni pekee, lakini kwa sasa kutokana na mwamko kuengezeka wananchi wamekuwa wakijitokeza kwa wingi katika kufuata huduma ya matibabu.

Hivyo, aliwapongeza viongozi wa shule hiyo kwa kujali wanafunzi wao sambamba na kuwapongeza madaktari wa jumuiya hiyo ambao wamekuwa wakitoa matibabu kwa wananchi katika vijiji mbalimbali kwa lengo la kupunguza matatizo yanayowakabili wananchi yakiwamo wanayoyajua na wasiyoyajua.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**MARY ZEPHANIAH NYAMBELE** anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 369023** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/PHQ/R-B/268496/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JESCA EDWARD NGAMBI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0325/0036** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **LUGALO SEKONDARI** mwaka **2016.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **TAB/RB/6149/2020.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 44 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**JOSEPH WIGINA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**NEEMA MPANDA ELISANTE**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 Mwezi wa June, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 11 Mwezi wa May, 2021.

NAIBU MSAJILI

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**KUITWA SHAURINI KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA SHAURI NAMBA 26 YA MWAKA 2021.**

**KESI YA MADAI YA ARDHI KATI YA MAPULISHI HIMA( MWOMBAJI) DHIDI YA ESTER MADATA (MJIBU MAOMBI)**

Mapulishi Hima unatakiwa kuhudhuria katika baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya wilaya ya Maswa kwenye shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24/6/2021 saa 02.30 asubuhi. Unajulisha kwamba iwapo utakaidi kupokea wito huu au kupuuza bila udhuru wa maana na kushindwa kufika simu iliyopangwa ,Baraza litalazimika kusikiliza maombi hata upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri ya mwenyekiti wa Baraza la ardhi na nyumba la wilaya ya Maswa leo tarehe 24 mwezi wa tano mwaka 2021.

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA.

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 07/OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late CLARA ABEL SUMARI**

**By 1. NDESHUKURWA ABEL SUMARI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to Come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **25 day of 06/2021**

**Dated at Morogoro this 27 day of 05/2021**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**

Usimamizi wa Mirathi **NAMBA 136/2019**
Ombi la **SALIMU NG'ANZI MWALIMU** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu **NG'ANZI MWALIMU NG'ANZI.**
Watu wote wanaodai kuwa uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **16/12/2019** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe **04/12/2019.**

Sahihi ya Hakimu

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU ENOS SAMWEL NGUSSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC679BSF** aina ya **SANLAG** yenye Chasis **No. LBRSP-JB5XH9019631 na Engine No 17923636** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba GE/IR/3527/2019

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

FADHILI SHEMHILU ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC.577 ACE.CHASSIS NAMBA BSED2501130905551.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/R-B/227125/2021

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

KENETH GOTADI LUGOME ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC. 407 BLE.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/R-B/274073/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SABUNI TUMAINI OMBENI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 628 BGT** – NISSAN. ENGINE NUMBER; **TD27249144**. CHASSIS NO. **ARGE24010590**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: TAN/ TAN/RB /**266397/2021.**

## TANGAZO LA UKUMBI

UKUMBI WA HARUSI NI BURE PR COMPLEX ILIYOPO SINZA BARABARA YA SHEKILANGO KARIBU NA HOSPITAL YA PALESTINA INATOA 'OFFER'YA UKUMBI BURE KUANZIA WATU 600 NA KUENDELEA KUNA STANDBY GENERATOR NA FULL 'AC' MAPAMBO.CHAKULA ,VITI,MEZA,MC NA MZIKI NI JUU YAKO. VINYWAJI VINAPATIKANA UKUMBINI KWA BEI NAFUU. KARIBUNI SANA.

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mali yasimamishwa uanachama ECOWAS

**Accra,** GHANA

VIONGOZI wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), wametangaza kusimamisha uanachama wa Mali baada ya jeshi la nchi hiyo kufanya mapinduzi ya pili ndani ya miezi tisa.

Uamuzi huo wa kuchukulia hatua dhidi ya Mali umefikiwa na kutangazwa wakati wa mkutano wa dharura wa kanda ya ECOWAS uliofanyika mwishoni mwa wiki, mjini Accra nchini Ghana.

Viongozi wakuu 10 na mawaziri wa mambo ya kigeni watatu wa mataifa wanachama wa ECOWAS, walihudhuria mkutano huo na katika tamko la mwisho, walisema wana wasiwasi mkubwa na hali ya usalama kwenye eneo la Afrika Magharibi kutokana na kile kinachoendelea nchini Mali.

**Viongozi watakaounda serikali ya sasa ya mpito hawataruhusiwa kuwania katika uchaguzi huo wa mwakani.**

Kupitia taarifa kuhusu maazimio ya mkutano huo iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ghana, Shirley Attorkor, uanachama wa Mali utasitishwa hadi Februari 2022.

Alisema huo ni muda uliopangwa kwa taifa hilo kufanya uchaguzi na madaraka kukabidhiwa kwa serikali ya kiraia itakayochaguliwa kidemokrasia.

Viongozi hao wa ECOWAS wameutumia mkutano wao kulaani kwa matamshi makali mapinduzi ya kijeshi yaliyofanywa Jumatatu wiki iliyopita, nchini Mali na kutoa rai ya kurejeshwa kwa utawala wa kiraia haraka iwezekanavyo.

Zaidi, Attorkor alisema moja ya maamuzi ya wakuu wa nchi, ni kwamba ni lazima katika siku chache zijazo wateue waziri mkuu, asiye mwanajeshi atakayeunda serikali ya mpito kwa kipindi kilichosalia, kwa maana umebakia miezi nane tu, muda wa mwisho waliopewa.

Muda huo wa mwisho ni Februari mwaka 2022 kutakapoitishwa uchaguzi na ECOWAS, ilisema viongozi watakaounda serikali ya sasa ya mpito hawataruhusiwa kuwania katika uchaguzi huo wa mwakani.

Licha ya kupendekeza hatua kadhaa za kuchukuliwa hivi sasa, ECOWAS haijasita kulinyooshea kidole cha lawama jeshi la Mali, kwa kurejesha nyuma juhudi za kuleta uthabiti kwenye taifa hilo.

Juhudi hizo ni pamoja na makubaliano yaliyofikiwa Septemba mwaka uliopita, mwezi mmoja tangu jeshi lilipofanya mapinduzi ya kwanza, yaliyoongozwa na Kanali Assimi Goita, ambaye sasa ndiye rais wa mpito wa Mali, baada ya kufanyika mapinduzi mengine wiki iliyopita.

Taarifa ya ECOWAS, pia ilitoa wito wa kuachiwa haraka kwa viongozi wanaoshikiliwa na jeshi.

Viongozi hao wanajumuisha rais wa mpito aliyelazimishwa na jeshi kuondoka madarakani, Bah N'Daw na waziri mkuu wake, Moctar Ouane, ambao wote wamewekwa kwenye kizuizi cha nyumbani tangu mapinduzi.

Pamoja na hali ya wasiwasi inayoendelea, viongozi wa ECOWAS wamehimiza wadau wa kimataifa ikiwamo Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Ulaya (EU), kuendelea kuiunga mkono Mali, kufanikisha utekelezaji wa kipindi cha mpito.

Mapinduzi ya kijeshi ya wiki iliyopita, yalichochewa na mabadiliko yaliyofanywa na rais wa mpito ambayo yaliwaondoa makamanda wa jeshi kwenye nyadhifa kadhaa, yamelaaniwa na jumuiya ya kimataifa na kufufua wasiwasi mkubwa juu ya usalama wa Mali na kanda nzima ya Sahel. **DW**

## Ndayishimiye ziarani Kenya

**Bujumbura,** BURUNDI

RAIS wa Burundi, Evariste Ndayishimiye (pichani chini), anaanza ziara ya kikazi ya siku mbili, nchini Kenya.

Kwenye ziara, hatua ya kwanza ya ziara yake itaanzia mjini Kisumu, Magharibi mwa Kenya. Kulingana na taarifa ya Ikulu ya Kenya, Rais Ndayishimiye ataambatana na mkewe Angelina Ndayubaha katika ziara hiyo, watashiriki katika zoezi la uzinduzi wa miradi mbalimbali ya serikali katika kaunti ya Kisumu.

Mbali na hayo, rais atakuwa mgeni wake, Rais Uhuru Kenyatta, atapoongoza taifa katika kuadhimisha sherehe za 58 za Siku ya Madaraka, uwanja mpya wa kimataifa wa Jomo Kenyatta, eneo la Mamboleo, Kaunti ya Kisumu. Sherehe zitafanyika huku kanuni za kitaifa za kukabiliana na Covid-19 zikizingatiwa.

Taarifa zaidi kutoka Ikulu ya Kenya, zinaeleza kuwa wake wa viongozi hao, Margaret Kenyatta na Angeline Ndayubaha, watahusika katika programu kadhaa ambazo maelezo yake yatafahamishwa kupitia vyombo vya habari.

Hii ni ziara ya kwanza ya Rais Ndayishimiye, nchini Kenya tangu alipopewa hatamu ya uongozi mwaka jana. Hivi karibuni alikuwa nchini Uganda, pamoja na mambo mengine alishiriki sherehe za kuapishwa kwa Rais Yoweri Kaguta Museveni. **RFI**





Mzee akifurahia jambo na watoto, jijini Beijing, mapema Mei 10, mwaka huu. Chama cha Kikomunisti China, jana kililegeza sharti la kuzaa watoto wawili na kuruhusu watoto watatu kwa wanandoa, ili kuinua idadi ya watoto, vijana kuendana na mahitaji ya sasa. **PICHA: AFP**

# China yaondoa sera ukomo kuzaa watoto

**Beijing,** CHINA

CHINA sasa imewaruhusu watu kuwa na hadi watoto watatu baada ya kupungua kwa kiwango cha watoto wanaozaliwa nchini humo.

Hatua hiyo ni mabadiliko makubwa ya kisera kwa serikali ya nchi hiyo.

Shirika la habari linalomilikiwa na serikali Xinhua, lilisema uamuzi huo, ulitangazwa jana katika mkutano wa viongozi wakuu wa chama cha kikomunisti.

Tangazo hilo, linajiri baada ya matokeo ya hesabu ya watu inayofanyika kila baada ya miaka 10, kuonyesha kwamba ukuaji ni mdogo sana katika miongo iliyopita.

Hatua hiyo imeshinikiza Beijing kubadilisha sera ili kuwaruhusu watu kuwa na watoto watatu.

China, ilifutilia mbali sera yake ya mtoto mmoja mwaka 2016, na kuibadilisha na kikomo cha watoto wawili ambacho kimeshindwa kusababisha kuongezeka kwa idadi ya watu.

Gharama ya kulea watoto katika miji imezuia wanandoa wengi wa China kuwa na watoto zaidi.

Hatua hiyo ya hivi karibuni iliidhinishwa na Rais Xi Jinping katika mkutano wa viongozi wakuu wa kisiasa shirika la habari la serikali lilisema kutakuwa na hatua za kuunga mkono.

Xi alisema hatua hizo zitasaidia kuboresha muundo wa idadi ya watu wa nchi, kutimiza mkakati wa nchi kukabiliana kikamilifu na idadi ya watu waliozeeka na kudumisha faida na utoaji wa nguvu kazi.

Wataalamu wengine walikuwa na wasiwasi juu ya athari ya sera hiyo, ikiwa kulegeza sera ya idadi ya watoto kungekuwa na ufanisi, sera ya sasa ya watoto wawili inapaswa kudhibitishwa kuwa na ufanisi pia.

Hao Zhou, mchumi mwandamizi huko Commerzbank, aliiambia Reuters: Lakini ni nani anataka kuwa na watoto watatu? Vijana wanaweza kuwa na watoto wawili, iwapo ni wengi. Suala la msingi ni gharama ya maisha ni kubwa sana na shinikizo za maisha ni kubwa sana." **BBC**

# LEONARDO AMKUMBATIA POCHETTINO KUONDOKA PSG



**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa michezo wa Paris Saint-Germain, Leonardo amesisitiza "ana furaha sana" kuwa na Mauricio Pochettino, licha ya ripoti kwamba kocha huyo anataka kuondoka klabuni hapo.

Imedaiwa kwamba, Pochettino, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kutoka kwa Thomas Tuchel hapo Parc des Princes Januari, aliiambia miamba hiyo ya Ligue 1 kwamba anataka kuvunja mkataba wake na timu hiyo.

Kocha huyo raia wa Argentina, ambaye mkataba wake unamalizika mwakani huku kukiwa na kipengele cha kuongeza miezi 12, amekuwa akihusishwa na kurudi Tottenham au kwenda Real Madrid kuchukua mikoba ya Zinedine Zidane.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinasema kwamba, Pochettino angependa kubaki hapo PSG kwa msimu mmoja zaidi.

Akizungumza na Europe1, Leonardo alisema: "Mauricio Pochettino ana mkataba wa miaka miwili na PSG na tuna furaha kubwa na yeye."

Uvumi kumhusu Pochettino umeibuka baada ya kushindwa kuiongoza PSG kutetea taji la Ligue 1, huku Lille wakilibeba taji la Ligi Kuu ya Ufaransa kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miezi 10.

Pia walifungwa na Manchester City kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakipoteza pia kwenye fainali ya michuano hiyo dhidi ya Bayern Munich katika fainali msimu uliopita.

# 'Kante kiungo mkabaji bora zaidi duniani'

**LONDON,** England

HAKUNA kiungo mkabaji bora zaidi kama, N'Golo Kante, kwa mujibu wa mchambuzi wa masuala ya soka, Martin Samuel.

Kante ndani ya miaka mitano ya hivi karibuni ametwaa mataji sita huku akiwa katika ubora wake uleule.

Kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mbele ya Manchester City aliweza kukata umeme kwa asilimia 100 bila kusababisha hata faulo moja.

Samuel amesema kuwa Kante ana nafasi ya kuweza kuingia kwenye vita ya kuwania tuzo ya Ballon d'Or kwa mwaka 2021 bila mashaka pamoja na Robert Lewandowski ambaye amefunga jumla ya mabao 41 kwenye Ligi Kuu Ujerumani.

Kante ameshinda Kombe la Dunia akiwa na timu yake ya Ufaransa, ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ameshinda taji la Europa na ana mataji mawili ya Ligi Kuu England pamoja na taji moja la FA akiwa chini ya makocha watano tofauti.

Samuel amesema: "Unaweza kuona namna gani anafanya na kwa uwezo wake kwa sasa hakuna ambye anafanya kama yeye hasa kwa namna ambavyo anajali wengine kuliko yeye binafsi, wapo wengi ambao walikuwa bora ila yeye anaonyesha uimara wake katika mapambano."





# *Benzema ammwagia sifa Mbappe*

**PARIS,** Uswisi

KARIM Benzema amemsifia Kylian Mbappe ambaye sasa atacheza naye kwenye michuano ya Euro 2020, kuwa ni mchezaji wa aina yake.

Benzema ameitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa, ambaye huenda akaanza naye kwenye nafasi ya ushambuliaji ya kikosi hicho.

"Sipendi kulinganisha wachezaji, lakini (Kylian) Mbappe ni mchezaji wa aina yake," alisema Benzemba katika mahojiano na Jarida la France Football.

"Uzuri kwamba yeye bado ni kijana mdogo, hivyo atakuwa na wakati mzuri zaidi kwa siku za usoni.

"Tayari nimefanya mazoezi naye. Tunacheza kwa kugusa mara moja, ana harakati nzuri, ana kasi kubwa na ana ustadi mbele ya lango."

Pia amemshukuru kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps, kwa kumuita katika kikosi hicho.

"Nadhani tayari nimesema. Lakini je! Unataka niseme tena? Aksante Didier.

"Tulikuwa tumezungumza wakati huo na tulibadilishana maneno. Nina furaha kurudi."

Benzema anahisi kurudi kwake katika timu ya taifa ilikuwa kwa bidii yake mwenyewe na imani.

"Nadhani ni kwa sababu ya kiwango changu na kwamba sijawahi kuacha kuamini. Nilikuwa nimeshuka kwa sababu ya kimaadili ilikuwa ngumu kutokuwa katika timu ya taifa," alisema.

## HABARI MICHEZO

# Copa Amerika 2021 mambo magumu

**BUENOS AIRES,** Argentina

MICHUANO ya Copa Amerika 2021 (Michuano ya Mataifa ya Amerika Kusini) imeachwa bila muandaaji zikiwa zimebakia wiki mbili kabla ya kuanza, baada ya Argentina kunyang'anywa nafasi hiyo.

Argentina ilipanga kuandaa michuano hiyo pamoja na Colombia, ambao waliondolewa Mei 20 kwa sababu ya maandamano nchini humo.

Shirikisho la soka la Amerika Kusini, (Conmebol) lilisema Argentina imeondolewa kwa sababu ya "hali ya sasa".

Kwa sasa nchi ya Argentina ipo kwenye wakati mgumu kutokana na maambuzi ya virusi vya corona kuongezeka maradufu zaidi.


Serikali za nchi nyingi za Amerika Kusini zimekuwa zikipinga kuandaa mashindano hayo kwa hali ya sasa na Argentina nayo imeondolewa kwa sababu hiyo, huku straika wa Uruguay, Luis Suarez akiripotiwa Ijumaa akisema kwamba kwa sasa kipaumbele kiwe kwa "afya ya binadamu."

Conmebol imesema kwa sasa "tunachambua nchi yenye nia ya kuandaa" ambazo zilionyesha nia ya kuandaa mashindano hayo yanayoshirikisha mataifa 10 kutoka Amerika Kusini, ambayo yalipangwa kuanza Juni 13 hadi Julai 10.

Shirikisho hilo lilitarajiwa kukutana jana, Jumatano kwa ajili ya kuteua nchini itakayoandaa michuano hiyo, ambayo ilishindikana kufanyika mwaka 2020 kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Brazil ndiyo bingwa mtetezi ambaye alishinda taji hilo mwaka 2019.

# XHAKA: FAHARI MOURINHO KUNIWANIA



**LONDON,** England

GRANIT Xhaka anajisikia "fahari" kusikia kwamba anawaniwa na kocha mpya wa AS Roma, Jose Mourinho, lakini kiungo huyo wa Arsenal amesisitiza kwa sasa anafikiria zaidi michuano ya Euro 2020.

Kocha wa zamani wa Tottenham, Mourinho aliteuliwa kuchukua nafasi ya Paulo Fonseca pale Roma baada ya kufukuzwa Spurs Aprili, mwaka huu, ambapo sasa ataanza kazi msimu wa mpya wa 2021/22/.

Na sasa Xhaka anaonekana kuwa kwenye rada za Mourinho katika usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto. Xhaka ametumia misimu mitano akiwa Arsenal tangu alipojiunga nayo akitokea kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Borussia Monchengladbach, ingawa nyota huyo wa kimataifa wa Uswisi hajawa maarufu sana kwa mashabiki wa klabu hiyo.

Xhaka tayari yupo na kikosi cha Uswisi kinachojiandaa na michuano ya Euro 2020, na ameliambia Jarida la Ujerumani la Blick: "Bila shaka nimesoma kuhusu uvumi wa mimi kutakiwa. Lakini kwa sasa akili yangu inafikiria zaidi timu ya taifa."

Alipoulizwa kuhusu kuwa kipaumbele kwa kocha Mourinho, Xhaka alijibu: "Kiukweli sijasikia nini ambacho Mourinho amesema, lakini hilo linanifanya nijisikie fahari.

# *Silva amshukuru Lampard Chelsea*

**LONDON,** England

THIAGO Silva amedai kuwa mbuzi wa kafara wakati wa kipindi chake cha kucheza Paris Saint-Germain na amemshukuru Frank Lampard kumsajili Chelsea mwaka jana.

Mlinzi huyo wa kati wa Brazil alikuwa akizungumza baada ya Blues kushinda bao 1-0 dhidi ya Manchester City Jumamosi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pale katika dimba la Do Dragao nchini Ureno.

Silva alikuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuichezea Chelsea kwenye fainali ya mashindano hayo ya Klabu Ulaya, akiiipiku ile ya Claude Makelele, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 alicheza kwa dakika 39 tu kabla ya kuumia.

Pia ni mchezaji wa tano kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu mitano mfululizo akiwa na timu tofauti, baada ya Marcel Desailly, Paulo Sousa, Samuel Eto'o na Alvaro Morata.

Kai Havertz alifunga bao pekee kwenye mchezo huo pale jijini Porto dakika tatu baada ya Silva kuondoka dimbani na Chelsea kuwa klabu ya tatu ya Uingereza kubeba taji hilo zaidi ya mara moja, baada ya Manchester United na Liverpool.

"Huu ni wakati muhimu zaidi katika maisha yangu ya soka," alisema akiiambia RMC Sport.

"Ni jambo lisilosahaulika. Sikuweza kutwaa taji hili nikiwa na PSG, lakini kesho nina furaha. Natumaini PSG nao watafanya hivyo siku moja."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAKAA MGUU SAWA KUMSAJILI LUKAKU

Inter pia ipo kwenye hatari ya kumpoteza Lautaro Martinez, Achraf Hakimi ambao...

**LONDON,** England

CHELSEA inapanga kufanya usajili wa nyota wa Inter Milan, Romelu Lukaku, kwa mujibu wa The Guardian.

**Lukaku kwa mara ya kwanza alicheza soka la Uingereza kati ya mwaka 2011 na 2014 wakati alipojiunga na Chelsea.**

Na sasa anaweza kurudi tena Chelsea baada ya kutokuwa na sintofahamu kuhusu majaliwa yake pale Inter.

Lukaku, ambaye alijiunga na 'Blues' hao mwaka 2011kabla ya kuondoka mwaka 2014, ameripotiwa kwamba anafikiria kuhusu majaliwa yake baada ya kocha Antonio Conte kuondoka klabu hapo.

Conte ambaye aliiongoza Inter kutwaa taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 10, aliondoka kutokana na kutoafikiana na uongozi kuhusu masuala ya kifedha.

Inter pia licha ya kuwa kwenye hatari ya kumpoteza Lukaku, nyota wake, Lautaro Martinez, Achraf Hakimi wamekuwa wakihuishwa na Paris Saint-Germain – na Alessandro Bastoni pia anaweza kuuzwa na 'Nerazzurri' hao.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO KUBAKI PSG

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kuendelea kubaki na Mauricio Pochettino kama kocha wa klabu hiyo wakati Real Madrid wakijiunga na Tottenham katika kumwania. (Mirror)

### XHAKA AMFURAHIA MOURINHO

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28, amesema anajisikia fahari kuwaniwa na kocha mpya wa AS Roma, Jose Mourinho, lakini ana furaha kuchezea kwa 'Washikabunduki' hao wa London. (Blick via Goal).

### DYBALA NA MKATABA MPYA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Paulo Dybala, 27, anajiandaa kufanya mazungumzo mapya na Juventus, huku kocha mpya Massimiliano Allegri akiwa na shauku na mustakabali wa kudumu na mchezaji huyo baada ya kurejea Turin. (Goal)

### ARSENAL HATIHATI KWA TOMAS

NAFASI ya Arsenal kumsajili mshambuliaji kutoka Sporting Lisbon, Tiago Tomas, 18, iko kwenye hatihati baada ya 'Washikabunduki hao kushindwa kufuzu michuano ya Europa. (Sun)

### MORENO AGOMBEWA ULAYA

MSHAMBULIAJI wa Villarreal, Gerard Moreno, 29, anazivutia West Ham, Newcastle na AS Roma. (Calciomercato)

### AURIER KUONDOKA SPURS

MLINZI wa Tottenham Hotspur, Serge Aurier, 28, amesema anajiandaa kuachana na klabu hiyo, msimu huu wa kipindi cha majira ya joto, huku PSG na AC Milan zikiwa timu zinazovutiwa na mchezaji huyo. (L'Equipe)

### UNITED, SANCHO MAMBO SAFI

MANCHESTER United wamefikia makubaliano binafsi na Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, lakini bado hawajatoa ofa rasmi kwa Borussia Dortmund ili kumsajili winga huyo wa England. (Sport1, via Star)

### TUCHEL KUPEWA MKATABA

THOMAS Tuchel anakaribia kusaini mkataba mpya baada ya kuiongoza Chelsea kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo raia huyo wa Ujerumani anaweza kukaa hapo hadi mwaka 2023 na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi. (Guardian)

### NIGUEZ AITAKA MAN UNITED

KIUNGO wa kati wa Atletico Madrid, Saul Niguez, 26, atashinikiza kuhamia Manchester United mbele ya Juventus au Paris St-Germain katika dirisha hili la usajili wa majira ya joto. (Mirror)

### WIJNALDUM BADO ANAAGA

KIUNGO wa Uholanzi, Gini Wijnaldum, 30, bado hajaenda Barcelona, kwani anaendelea kuaga Liverpool. (ESPN Netherlands via Liverpool Echo)

## HABARI MICHEZO

### 'Hakuna pingamizi wagombea TAWFA'

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Kamati ya Uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TAWFA), George Mushumba, amesema hakuna pingamizi lolote walilopokea kwa wadau wa mchezo huo kuelekea uchawguzi huo unaotarajiwa kufanyika Juni 26, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mushumba alisema baada ya wagombea kuchukuwa fomu kulikuwa na zoezi la kupokea na kusikiliza pingamizi ambalo limefanyika Mei 27 hadi 28 na 29 kulikuwa na usaili baada ya kutopokea pingamizi.

"Mchakato umeenda vizuri na tumefanya usaili kwa uhakika kwa wagombea ambao wanawania nafasi mbalimbali kwenye uchanguzi na sasa wanatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa kama tulivyoanza salama hadi kufikia sasa," alisema Mushumba.

Wagombea ambao wameingia kwenye uchanguzi huo, nafasi ya Mwenyekiti wako wawili ambao ni Amina Karuma anayetetea nafasi yake na Sara Chao, Makamu Mwenyekiti nayo wapo wawili, Roseleen Kisiwa na Beatrice Mgaya wakati nafasi ya Katibu Mkuu, Somoe Ng`itu anayetetea nafasi yake hana mpinzani sambamba na Katibu Msaidizi, Veronica William.

### Pamba, Transit Camp zapangiwa wapinzani

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa zamani wa Ligi Kuu ya Muungano, Pamba FC ya Mwanza, mechi ya mchujo 'Play off', itamenyana na timu itakayomaliza nafasi ya 13 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kuwania kupanda ligi hiyo msimu ujao.

Katika droo iliyochezeshwa juzi Dar es Salaam, Transit Camp itamenyana na timu itakayomaliza nafasi ya 14 kwenye Ligi Kuu msimu huu huku mechi za kwanza zikichezwa Julai 21 na timu hizo za Daraja la Kwanza zote zitaanzia nyumbani kabla ya kusafiri kuzifuata timu za Ligi Kuu kwenye mechi za marudiano Julai 24.

Mbeya Kwanza na Geita Gold zimepanda moja kwa moja baada ya kuongoza makundi yao, A na B, wakati Transit Camp na Pamba zinapitia kwenye mchujo baada ya kumaliza nafasi ya pili.

# WAZIRI ATUMA SALAMU CAF KUPITIA NAMUNGO, SIMBA

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, ametuma salamu kwa klabu kubwa zitakazoshiriki michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kuwa timu za Tanzania si uchochoro wa kupita.

**Bashungwa aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akisoma makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 kiasi cha Sh. bilioni 54.7 ambazo Bunge limeziidhinisha.**

Katika hotuba yake, waziri huyo alizipongeza klabu ya Simba na Namungo kwa kuwezesha soka nchini kukua kimataifa kwa ngazi ya klabu baada ya kufanya vizuri.

Alisema mafanikio hayo kwa pamoja yameipa nchi fursa ya kuingiza klabu nne kwenye michuano hiyo ya CAF; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Bashungwa alisema serikali itaendelea kuweka mazingira bora zaidi yatakayochochea mafanikio makubwa zaidi ya mpira wa miguu na michezo mingine katika nyanja za kimataifa.

Alisema mafanikio yaliopatikana katika mpira wa miguu ni Klabu ya Simba kuingia robo fainali katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Klabu hii imeonyesha soka la hali ya juu katika mashindano hayo, kwani ilizichakaza klabu kubwa barani Afrika kama vile FC Platinum ya Zimbabwe kwa mabao 4-0, Al Merreikh ya Sudan mabao 3-0, As Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo 4-1, Al Ahly ya Misri bao 1-0 na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini 3-0," alisema.

Alisema timu ya Namungo ambayo iliiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika katika hatua za awali ilizichabanga Al-Rabita ya Sudan Kusini mabao 3-0, Al Hilal Obeyid ya Sudan 5-3 na De Agosto ya Angola mabao 7-5.

Kadhalika, alisema wizara itawajengea uwezo wasanii kimitaji na mafunzo kupitia mfuko wa utamaduni na sanaa, hatua ambayo itaongeza tija, ubora na ushindani wa kazi za sanaa na wabunifu wa ndani kitaifa na kimataifa.

Pia alisema wizara yake itakamilisha uundwaji na kuanza matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kuwahudumia wasanii na wadau wengine wa sanaa ili kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma, kurahisisha urasimishaji wa Sekta ya sanaa na shughuli za ubunifu na kubwa zaidi, kuongeza mapato ya wasanii na serikali.

**MABINGWA...**



Wachezaji wa timu ya Geita Gold, wakishangilia na Kombe la ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza baada ya kulitwaa juzi katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kwa kuifunga Mbeya Kwanza katika mechi ya fainali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mlandege, Hard Rock vitani kujinasua

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya Ligi Kuu ya Zanzibar kuelekea ukingoni huku tayari bingwa akiwa amepatikana, vita sasa vimebaki kwa timu zinazoburuza mkia kupambana kuepuka kushuka daraja msimu huu.

Timu mbili zitakazoshuka daraja zitajulikana katika mechi za leo ambapo ndizo zitakazotoa taswira nani atabaki Ligi Kuu na atakayeaga michuano hiyo kwenda kucheza Ligi Daraja la Kwanza.

KMKM tayari imetwaa ubingwa baada ya Jumamosi kuifurusha Polisi kwa bao 1-0 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Amaan, hivyo sasa vita vipo kwa upande wa timu ambazo zipo katika hatari ya kushuka daraja msimu huu, Hard Rock ambayo inaburuza mkia ikiwa na alama 19 na aliyekuwa bingwa mtetezi, Mlandege ambayo inaalama 22 ikishika nafasi ya pili kutoka mkiani.

Timu nyingine inayoweza kuzama na jahazi hilo ni Chuoni ambayo ina alama 23 katika nafasi ya tatu kutokea mkiani, hivyo zote tatu zinapaswa kushinda michezo yao miwili iliyobaki ili kujihakikishia kusalia Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Kwa upande wa timu ambazo zinapaswa kushinda mchezo mmoja ili kusalia Ligi Kuu msimu ujao ni JKU, Polisi na Black Sailor ambazo zote zina alama 24.

Timu ya JKU itashuka Dimba la Amaan leo kuumana na Hard Rock inayohitaji kushinda michezo yake yote miwili wakati wapinzani wao hao ushindi wa mechi hiyo ukiwahikikishia kusalia Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa timu ya JKU, Omar Khamis "Matu", alisema maandalizi ya kuelekea mchezo huo kwa upande wa wachezaji wake yamekamilika. Alisema kikosi chote cha kwanza kitashuka uwanjani ili kuzisaka alama tatu na kujihakikishia wanabaki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

"Hatuangalii tu kushinda mechi moja, bali zote mbili kwani tunahitaji kushinda, maana hatujui timu tulizofungana nazo alama zitapata matokeo katika michezo yao ama la. Hivyo tumejiandaa kuvuna alama sita katika mechi mbili zilizobaki," alisema

Mchezo mwingine utakaopigwa leo utakuwa kati ya Polisi na Mlandege katika Dimba la Mau, Michezo yote ikichezwa majira ya saa 10:00 alasiri.

Ligi Kuu Zanzibar msimu huu imeshirikisha timu 12 na mbili zitakazoburuza mkia zitashuka daraja.

Michezo

Jumanne Juni 1, 2021

Nipashe



Chelsea mguu sawa kumsajili Lukaku UKURASA 22

ZAWADI..



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimkabidhi zawadi (Zanzibar Door), beki wa Crystal Palace inayoshiriki Ligi Kuu England, Mfaransa Mamadou Sakho na mkewe, Majda, baada ya kumtembelea Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mamadou Sakho aleta neema soka Zanzibar

●●● Beki huyo kisiki wa Crystal Palace ya England, ametinga Ikulu na kuteta mazito na Rais Mwinyi, akiahidi...

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BEKI kisiki wa kati wa Klabu ya Crystal Palace inayoshiriki Ligi Kuu England (EPL), ambaye ameichezea timu ya Taifa ya Ufaransa kuanzia za vijana hadi ya wakubwa, Mamadou Sakho, ametua visiwani hapa na kisha kumtembelea Ikulu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, huku akiahidi mambo makubwa.

**Mchezaji huyo ambaye ametua visiwani hapa tangu Jumamosi ya Mei 29, mwaka huu kwa ziara ya kitalii ya siku nne, maalum kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar, ameambatana na familia yake akiwamo mkewe, Majda Sakho, ambao kwa pamoja jana walimtembelea Rais Dk. Mwinyi Ikulu.**

Sakho ambaye ameambatana na timu ya waandishi wa habari wa Televishen ya TF1 ya nchini Ufaransa, kwa lengo la kutengeneza makala maalumu ya ziara yake itakayotumika kuutangaza utalii wa Zanzibar nchini Ufaransa hususan maeneo ya vivutio vya utalii alivyotembelea, alimweleza Dk. Mwinyi azma yake ya kuanzisha kituo cha kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana Zanzibar.

Alisema ameamua kuchukua hatua hiyo ya kuanzisha kituo cha kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana Zanzibar kwa kutambua kwamba ana deni na wajibu mkubwa wa kuleta maendeleo Afrika akijua kuwa yeye ni Mwafrika licha ya kwamba amezaliwa Ufaransa na anabeba uraia wa taifa hilo.

Alifafanua kuwa ameichagua Zanzibar kuwa ni eneo maalum kwa kuanzisha kituo hicho kitakachoendeleza soka nchini na kwamba vipaji vitakavyoibuliwa katika kituo hicho itakuwa ni alama maalum aliyoiacha katika kuinua soka na kuithamini asili yake.

"Ninapokuwa Ulaya si wengi wanaoniuliza unatoka nchi gani ya Ulaya, bali huniuliza ninatoka nchi gani ya Afrika, najivunia asili yangu ya Afrika, hivyo nimeamua kuifanyia kitu na nimeichagua Zanzibar," alisisitiza.

Sambamba na hayo, Sakho alieleza jinsi alivyovutiwa na mazingira na anavyoipenda Zanzibar kutokana na ukarimu wa watu wake, mazingira pamoja na utamaduni wake huku akiahidi azma yake ya kujifunza lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa Rais Mwinyi, ameipongeza azma ya mchezaji huyo ya kuanzisha kituo cha kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana Zanzibar na kwamba huo ni mwanzo mzuri katika kuinua michezo visiwani hapa.

Rais Dk. Mwinyi alimpongeza Sakho kwa kuitembelea Zanzibar kwa mara ya pili huku akimweleza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana naye katika kuanzisha kituo hicho cha kuendeleza vipaji vya michezo kwa vijana.

Aidha, baada ya kuzungumza na Rais Mwinyi, mchezaji huyo pia alipata fursa ya kufanya mahojiano na waandishi wa habari waliohudhuria mazungumzo hayo ambapo alielezea utayari wake wa kuwa Balozi wa Hiari wa Kuutangaza Utalii wa Zanzibar.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Leila Muhamed Mussa, alisema: "Hivyo tunaposema neema tupu sasa tutambue kwamba hizo ndio neema zenyewe tunazozisema". Familia ya beki huyo Juni mwaka 2017 wakati huo Sakho akiichezea Liverpool ya England, ilitembelea Zanzibar na moja ya maeneo ilikuwa ni kituo cha kulelea watoto yatima cha SOS kilichoko Mombasa, Unguja.

## TFF yakaliwa kooni bungeni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WABUNGE wamelikalia kooni Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kudai limekuwa na upendeleo katika mwenendo wa adhabu zake inazozitoa kwa viongozi wa klabu bila kuzingatia usawa.

Wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2021/22, walisema hata waamuzi nao wamejiingiza katika mambo hayo ya ovyo kwa kutoa adhabu za aina hiyo uwanjani.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, akichangia makadirio hayo alisema kutokana na kutokuwapo kwa usawa kiongozi mmoja akifanya makosa anapona na mwingine akirudia makosa haya hayo kesho anapewa adhabu za kutisha zaidi.

"Waamuzi wamejiingiza katika mambo hayo hayo ya ovyo kwa kufanya upendeleo uwanjani jambo ambalo linazikosesha klabu nyingine ushindi kwa sababu waamuzi wanaogopa watafungiwa," alisema huku akidai kuwa anapata mashaka ndani ya TFF kama kuna uadilifu na kuitaka serikali kusafisha mpira wa miguu ili kuleta matumaini yaliyotarajiwa.

Madai hayo yaliungwa mkono na Mbunge wa Manonga (CCM), Seif Gulamali, ambaye alisema baadhi ya viongozi wamekuwa na tatizo katika kusimamia ligi na kueleza wengine wakishtakiwa kesho (TFF) wanakaa na hukumu inatoka.

"Lazima kuwe na shirikisho ambalo halina unazi ambalo kiongozi anaweza kuwa na timu yake, lakini inapofika suala la kusimamia michezo haweki unazi wake," alisema.

Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi, aliitaka TFF kuangalia kanuni zao ili kuwe na adhabu ambazo ni rafiki zinazoweza kumjengea mtu kurekebika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >